UKURASA WA 4
**Mchakato** kufumua Sheria ya Mtoto waanza Zanzibar

UKURASA WA 11
**Hatari** kujitwika majukumu ya watu wengine

UKURASA WA 11
MAISHA NDIVYO YALIVYO
**Mke** akimbia familia, aishi klabu za usiku





# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 22, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581471

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


UKURASA 9

# MAJONZI

• **Ajali** ilivyokatisha uhai wa watu 18, kujeruhi 35... *Endelea ukurasa 3*




Wananchi wakiangalia mabaki ya basi la Kampuni ya Alfa lililokuwa linatokea Mwanza kwenda Dar es Salaam na lori la mafuta, baada ya kugongana mkoani Tabora jana. **PICHA: MTANDAO**

## Muhimbili yajitosa kuwatibu wanaume wenye matiti

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akikagua magari na mitambo ya uchimbaji madini katika hafla ya uzinduzi wa mitambo hiyo iliyonunuliwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) jijini Dodoma jana. Kulia kwake ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko na (kushoto kwake) ni Waziri wa Madini, Anthony Mavunde. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Samia aanika siri uteuzi wa Biteko

• **Mwenyewe** ampa angalizo Mavunde... *Uk. 2*

**MICHEZO** **YANGA, AZAM FC KAMILI KUMALIZANA** UK.24 **KATUNI** UK.6




Wakazi wa Kwa Hakimu, Malamba Mawili Mbezi, wakiwa wameweka tangazo linalozuia pikipiki maarufu bodaboda kupita saa 6 usiku kwenye eneo hilo, baada ya kukithiri vitendo vya uporaji kwa kutumia vyombo hivyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia atoboa siri uteuzi wa Biteko

## • Aonya utoroshaji madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa siri ya uteuzi wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko. Amesema unatokana na kupaisha sekta ya madini katika kuchangia Pato la Taifa.

Mkuu wa Nchi pia ameeleza sababu za kumteua Anthony Mavunde kuwa Waziri wa Madini. Ni kutokana kuwa zao la madini (alikuwa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo kabla ya kuwa mbunge) na kusisitiza afanye nao kazi kwa ushirikiano kwa kuwa anajua lugha yao na kuwaelewa vizuri huku Dk. Biteko akimpa 'ujanja' namna ya kuendelea kubaki salama katika nafasi yake.

Jijini Dodoma jana wakati wa halfa ya kukabidhi mitambo ya uchorongaji kwa wachimbaji wadogo na vifaa vya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Rais Samia alisema "nimshukuru Biteko kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya sekta hii. Siku ninamwapisha kuwa Waziri wa Madini miaka miwili na nusu iliyopita, nilimwambia tumekupa dhima ya kuifanya sekta ya madini ifikapo 2025 ichangie kwa asilimia 10 kwenye Pato la Taifa.

"Dk. Biteko alifikisha asilimia 10 mwishoni mwa mwaka jana. Ametumia muda mfupi kuliko tulivyokadiria. Sasa nikaona mbinu ileile aliyotumia kule nimpandishe awe Naibu Waziri Mkuu, aje atusaidie huku, lakini nimkabidhi na (Wizara ya) Nishati aende kutusaidia kwenye nishati. Kwa hiyo, dokta (Biteko) pole na hongera."

Rais Samia alisema sekta ya madini inaendelea kuchangia Pato la Taifa kwa upande mmoja na uchumi wa wachimbaji wadogo kwa upande mwingine.

UTOROSHAJI MADINI

Mkuu wa Nchi pia alikemea vitendo vya utoroshaji madini vinavyofanywa na baadhi ya watu wasiokuwa wazalendo. Yeyote atakayekamatwa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria kama walivyochukuliwa hatua waliokamatwa hivi karibuni.

"Ninapenda kuwaasa kuachana na vitendo vya utoroshaji wa madini, hii sijui mnafanya kwa faida ya nani wakati ndani kuna viwanda vinaangalia malighafi?

"Pelekeni viwandani madini yakasafishwe yakaongezwe thamani tupate bidhaa tutakayouza kwenye masoko ya dunia.

"Huo si uzalendo wala sio utanzania, wale wenye tabia hiyo waache kwani viwanda vipo ndani na soko ni nzuri. Kama watu wameingia mkataba wawaambie kuwa hawaruhusiwi.

"Kama tukikukamata, waliokamatwa juzi wanafahamu kazi yetu. Tuchukue hatua za kujenga tasnia yenye uthabiti na uwajibikaji, si hila na ujanjaujanja, tufuate sheria, kanuni na miongozi iliyopo kuhakikisha rasilimali madini zinawanufaisha watu wote," aliagiza.

Rais Samia pia alibainisha umuhimu wa wachimbaji wadogo kupewa fursa na taasisi za fedha katika kuongezwa mitaji na kutaka taasisi za fedha ziwaamini kwa kuwa wanapowezeshwa ni sawa na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi pamoja na kutanua wigo wa walipakodi nchini.

Aliongeza kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wa wachimbaji wadogo katika kutoa ajira, kukuza uchumi na kipato. Serikali imekuwa inafanya jitihada kuboresha shughuli za uchimbaji mdogo.

Katika kutekeleza suala hilo kwa vitendo, alisema serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wachimbaji wadogo ambao watauza madini katika soko la ndani huku akisema serikali imeweka punguzo la asilimia mbili la mrabaha na asilimia moja ya ada ya ukaguzi wa madini, lengo likiwa wauze madini katika masoko yaliyomo nchini.

Alisema STAMICO imeanzisha vituo vya mfano Lwamgasa, Katente na Itumbi ambako kutokana na ufanisi wa vituo, shirika limeandaa mpango kupanua vituo hivyo vitoe huduma kwa watu wengi zaidi.

Kadhalika, alisema vituo vingine vitajengwa kwa ajili ya madini ya chokaa mkoani Tanga na Chumvi mkoani Lindi.

"Wakati wa ziara yangu Lindi nilielezwa moja ya changamoto ya wazalishaji chumvi Lindi na Mtwara ni kukosa soko la uhakika.

"Sasa changamoto hiyo inaelekea kupatiwa suluhisho na STAMICO kwa kujenga kiwanda cha chumvi na kuanzisha shamba darasa.

"Msiwasahau kinamama wa Singida ambao wamejiajiri katika uzalishaji chumvi, nilielezwa katika eneo hilo hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika hadi sasa na kama likipewa mkazo litaleta ufanisi kwa kuongeza kipato," alisema.

Rais alisema mpango wa serikali ni kufanya utafiti kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika eneo kubwa zaidi. Mkakati utasaidia kubaini kuwapo madini kwenye miamba na sekta mbalimbali kufaidika, hivyo mitambo iliyozinduliwa jana itakuwa chachu ya ukuaji shughuli za uchimbaji kwa kuwa zitapatikana taarifa za uhakika na wachimbaji kuacha uchimbaji wa kubahatisha.



**STAMICO ILIVYONUSURIKA**

Rais pia alisema shirika hilo kwa sasa lina mafanikio makubwa na linatoa gawio kwa serikali na kuelekeza kuwa kabla ya mafanikio hayo hali yake ilikuwa mbaya.

"Kila aliyekuwa akilikagua anasema 'limeshindwa, lifutwe, labda liundwe lingine'. Tukasema 'hapana, ngoja tufanye utafiti. Tulipoona upungufu tukachukua hatua za kuondoa upungufu na leo ninafarijika STAMICO imesimama yenyewe na inaleta fedha serikalini.

"Mashirika mengi yalikuwa badala ya kuleta fedha serikalini, yanakula serikalini. STAMICO imeweza kutafsiri kwa vitendo dhana ya mageuzi ambayo serikali imekuwa inayasisitiza," alipongeza.

Alisema mitambo ya uzalishaji mkaa mbadala itakayosambaza maeneo mbalimbali nchini, itasaidia mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira.

**KAULI YA BITEKO**

Awali, Dk. Biteko alisema "Mavunde amesema kuna mambo yamefanywa na msingi umewekwa. Haya yote hayajafanywa na Biteko, yamefanywa kwa maelekezo yako Rais.

"Ninataka nimwambie Waziri wa Madini, salama yake na kazi yake msikilize Rais atakachokuelekeza. Wasaidie wachimbaji wake kama unavyofanya. Nikuhakikishie kila aina ya ubunifu utakaokuwa nao na mimi nilipata bahati hiyo Rais atakupa nafasi ya kufanya kazi yako, ninaamini dira uliyokuja nayo baada ya muda tutaona ikitokea."

Naye Waziri Mavunde alisema ili sekta ya madini iendelee kuchangia mchango mkubwa, ni lazima utafiti ufanyike kuboresha kanzidata itakayobaini aina ya madini yaliyopo na namna ya kuyachimba.

Alibainisha kuwa, hadi sasa eneo lilofanyiwa utafiti ni asilimia 16 ambalo limechangia fedha za kigeni kwa mwaka fedha uliopita zaidi ya asilimia 56.

Akizungumzia mitambo iliyokabidhiwa, Mkurugenzi Mkuu wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema mitambo ambayo imezinduliwa jana ina thamani ya Sh. bilioni 9.2 huku uwekezaji ambao shirika limeufanya katika mwaka huu ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 17.3.

Alieleza kuwa mitambo mitano iliyozinduliwa ni sehemu ya mitambo 15 ambayo imenunuliwa na STAMICO itakayokwenda kuinua uchumi wa wachimbaji na taifa kwa ujumla.

**UHURU WA ZAMBIA**

Katika hatua nyingine, mwandishi wetu Halfani Chusi anaripoti kuwa Rais Samia anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi ya siku tatu Zambia kuanzia kesho, ikiwa na lengo la kujenga ushirikiano kati ya nchi hizo mbili zenye historia kubwa kidiplomasia.

Katika ziara yake hiyo, Rais Samia amekubali mwaliko wa kuwa mgeni rasmi katika sherehe za maadhimisho ya Miaka 59 ya Uhuru wa Zambia zitakazofanyika Oktoba 24 mwaka huu jijini Lusaka.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, aliwaambia waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa kipaumbele katika ziara hiyo ni pamoja na namna bora ya kuboresha miundombinu inayounganisha Tanzania na Zambia ili kufikia faida za kiuchumi.

Alisema ziara hiyo pia inategemewa kuangazia namna bora ya kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wafanyabiashara wa Tanzania na Zambia na kuibua fursa mpya za ushirikiano kati ya nchi hizo mbili kwa kuzingatia Zambia ni lango la bidhaa zinazotoka Tanzania kwenda Zimbabwe na Kongo.

## HABARI KITAIFA

# Ajali ilivyokatisha uhai wa watu 18

**Halima Ikunji na Benny Kingson,** NZEGA

WATU 18 wamefariki dunia na wengine 35 kujeruhiwa katika ajali iliyotokea eneo la Udomouchana, wilayani Nzega, mkoani Tabora ikihusisha basi la abiria na lori la mafuta.

Ajali hiyo ilitokea jana saa tano asubuhi huku chanzo kikidaiwa uzembe wa dereva wa lori la mafuta la Kampuni ya GBP lenye usajili wa namba T 481 ACB, kutaka kulipita gari la mbele yake bila kuchukua tahadhari na kuligonga basi hilo.

Wakati ajali hiyo inatokea, lori hilo lilikuwa linatokea Dar es Salaam kwenda Mwanza na basi la Kampuni ya Alfa lenye usajili namba T 612 CQD, lilikuwa linatoka Mwanza kwenda Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, akiwa katika eneo la ajali, alibainisha kuwa hadi wakati huo (mchana) waliothibitika kufariki dunia ni watu 18 na majeruhi 35 waliokuwa wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega.

Alibainisha kuwa kati ya waliofariki dunia, 13 ni wanaume na wanawake watano. Baadhi ya majeruhi alidai hali zao zilikuwa mbaya.

"Jeshi la Polisi bado tunaendelea na utaratibu wa kutambua taarifa za wote waliofariki dunia, pia kuwatambua majeruhi wote kwa majina yao, tutaendelea kuujulisha umma kadri tunavyopata taarifa," alisema Kamanda Abwao.

Alisema magari yaliyohusika katika ajali hiyo yameharibika vibaya na waliandaa utaratibu wa kuyaondoa barabarani ili watumiaji wengine wa barabara hiyo waendelee na safari.

Kamanda huyo alisema ajali hiyo imesababishwa na mwendo kasi na uzembe wa dereva wa lori ambaye 'alichepuka' bila kuchukua tahadhari na kuligonga basi hilo la abiria.

Baadhi mashuhuda wa ajali hiyo, walieleza kuwa gari hilo la mafuta lilikuwa katika mwendo kasi na kuelekea upande ambao si wake bila kuchukua tahadhari na kuligonga basi hilo upande wa kushoto wa dereva.

"Lori limeharibika sana, hatuna uhakika kama dereva wake atakuwa amepona au la kwa kuwa na yeye ni miongoni mwa waliopelekwa hospitalini," alisema Mussa Hussen aliyeshuhudia ajali hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Naitapwaki Tukai, alitoa pole kwa majeruhi wote na kuwataka Watanzania kuwa wavumilivu kwa kipindi hiki cha majonzi.

"Nimepokea taarifa hizi nikiwa katika maadhimisho ya miaka 100 ya Hospitali ya Misheni, nikasema lazima nifike kwenye eneo la tukio, ajali ni mbaya, tuwakumbushe madereva kufuata sheria wawapo barabarani," alisema Tukai.

# Muhimbili yajitosa kutibu wanaume wenye matiti

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) - Mloganzila, imesema huduma ya kupunguza uzito na upasuaji rekebishi zinazotarajiwa kufanyika hospitalini huko, zitahusisha pia wanaume wenye maumbile kama matiti.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji MNH-Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, alibainisha hayo jana na kueleza kuwa huduma hizo kama alivyoeleza awali, zitatolewa kwa siku mbili kuanzia Oktoba 27 mwaka huu.

"Huduma hii ya kupunguza uzito ni kwa jinsi zote mbili kwa kuwa kumekuwa na minong'ono kwamba, mbona mmependelea wanawake. Huduma itafanyika kwa watu wote wenye uzito mkubwa," alisema. Muhumba ambaye ni Daktari Bingwa wa Upasuaji alisema hata huduma rekebishi zitatolewa kwa wanaume na wanawake.

"Tumeona wanaume kwa bahati mbaya inatokea miili yao wanakuwa kama wana matiti badala ya kifua cha kiume, nao watafanyiwa upasuaji rekebishi katika siku hizi mbili," alisema.

Bingwa huyo aliwatoa hofu Watanzania kwa kuwaeleza kuwa, upasuaji huo ni salama na ni sawa na upasuaji mwingine unaofanywa hospitalini huko.

Alisema upasuaji huo utaongozwa na Daktari Bingwa Mbombezi wa Upasuaji wa Kupunguza Uzito na Kurekebisha Mwili, Mohit Bhandari kutoka India.

Aliwasisitizia wananchi wanaotaka kupata huduma hizo kuendelea kujiandikisha kwa kuwa mpaka sasa, huduma ya kupunguza uzito na kufanya upasuaji rekebishi imekamilika kwa kiasi kikubwa na itafanyika kwa tarehe tajwa.

Awali Dk. Muhumba, akifafanua kuhusu upasuaji huo, alisema wanaposema upasuaji wa kupunguza uzito, fasili yake ni upasuaji unaofanyika kwenye tumbo kwa kupunguza nafasi ya kuhifadhi chakula.

Alisema katika operesheni hizo, ziko za aina tatu: Kupunguza tumbo lenyewe kwa kukata sehemu ya tumbo au kuvuka sehemu ya kuhifadhi chakula na kukifanya kikitoka kwenye koo kwenda moja kwa moja katika utumbo mdogo na kushona tumbo na kubaki nafasi kidogo.

"Operesheni zote hizi zitafanyika. Kuhusu upasuaji rekebishi ni kupunguza mafuta katika tumbo au mama anataka kurekebisha matiti yake madogo au makubwa vyote vitafanyika au mkono umejaa nyama utarekebishwa.

"Huduma hii ya upasuaji rekebishi au kupunguza uzito hospitalini hapa gharama zake zitakuwa nafuu kulinganisha na zile za nje ya nchi," alisema.


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.104 OF 2023**
**IN the Matter of the late:**
**GODWIN ISEGELEKESYE MWANGOKA**

**By 1.SUZANA GODWIN MWANGOKA**
**2..............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 24 October 2023.

Dated at Morogoro this 12 day of October 2023.






**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

ABDUL I KISALU

Anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI (HAOJUE) yenye namba za usajili MC 957 CTC (CHASSIS NO.LC6PCJK20L0099669,

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi PHQ/MOR/MOR/4573/2023.



TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)** inapenda kuwataarifu waombaji kazi waliofaulu mtihani wa mchujo na kuchaguliwa **(SELECTED)** kwa ajili ya usaili wa vitendo na mahojiano **(Practical and Oral Interview)** unatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **29 Oktoba, 2023** hadi tarehe **2 Novemba, 2023** na hatimaye kuwaajiri watakaofaulu usaili huo. Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

i. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na **kitambulisho** kwa ajili ya utambuzi; vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Hati ya kusafiria au Leseni ya udereva;
ii. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **vyeti vyao halisi, kuanzia cheti cha Kuzaliwa, Kidato cha IV, VI, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu, Shahada** na kuendelea kutegemeana na sifa za mwombaji;
iii. Wasailiwa watakaowasilisha **"Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za Kidato cha IV na VI (Form IV and Form VI result slips) HAZITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI;**
iv. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi;
v. Kila msailiwa azingatie **tarehe** na **mahali** alipopangiwa kufanyia usaili kulingana na ratiba husika na muda wa kufika ni **saa moja kamili asubuhi**;
vi. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika **(kama TCU, NACTE au NECTA)**;
vii. Waombaji kazi ambao namba zao hazikuchaguliwa kwa ajili ya hatua inayofuata watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika.
viii. **Kwa kada ambazo wanatakiwa kusajiliwa na Bodi zao za Kitaaluma wanapaswa kuja na vyeti vyao Halisi vya Usajili pamoja na Leseni za kufanyia kazi (zilizo hai).**
ix. **Wasailiwa wote walioitwa kwenye usaili wahakikishe wanaingia kwenye akaunti zao na kunakili namba ya mtihani kwa kuwa namba hizo hazitatolewa siku ya usaili.**
x. Matokeo na ratiba ya usaili vinapatikana kupitia tovuti ya TRA www.tra.go.tz

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| Tovuti | : | **www.tra.go.tz** |
| Namba za simu bila malipo | : | **0800-780 078** au **0800-750 075 au 0800-110 016** |
| WhatsApp | : | **0744 23 33 33** |
| Barua pepe | : | **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na Utawala**

# Mchakato kufumua Sheria ya Mtoto waanza Zanzibar

- Adhabu kali zaidi wanaodhalilisha watoto

**Na Sabato Kasika,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanza mchakato wa kukusanya maoni ya kuifanyia maboresho Sheria ya Mtoto Na. 6 ya Mwaka 2011 ili iendane na wakati.

Mchakato huo unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikishirikisha wadau mbalimbali.

Mkurugenzi wa Idara hiyo, Siti Abass Ali, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha ukusanyaji maoni kilichofanyika katika Ukumbi wa Skuli ya Kidonge Chekundu.

Siti aliwataja baadhi ya wadau hao kuwa ni viongozi wa dini, wanasheria na Jeshi la Polisi, huku akifafanua kuwa kutokana na vitendo vinavyojitokeza katika jamii, ikiwamo ajira za utotoni, idara yake imelazimika kuipitia sheria hiyo na kuja na uamuzi wa kuifanyia maboresha ili iendane na wakati.

"Sheria hiyo imetusaidia na inaendelea kutusaidia, lakini tumeona ni vyema tuifanyie maboresho ili iwe bora zaidi," alisema Siti.

Alifafanua kuwa sheria inazungumzia umuhimu wa mtoto kupata haki zake za msingi ikiwamo kupata elimu, matibabu, chakula, malazi, malezi bora na namna ya kuepuka udhalilishaji. Kupitia wadau hao itaboreshwa zaidi.

Alisema wameanza kukusanya maoni ya makundi ya watoto kupitia mabaraza yao, viongozi wa dini, waandishi wa habari, waratibu wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

"Zitafuata wizara ikiwamo ya elimu, taasisi mbalimbali za umma na binafsi, kwa lengo kufanikisha kile ambacho tumekikusudia kwa ajili ya uboreshaji wa sheria hii," alisema.

Aliwataja wadau wengine watakaoshiriki mchakato huo kuwa ni Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (DPP), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Zanzibar (TAMWA-ZNZ) na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

"Marekebisho ya sheria hiyo yanatokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo kimsingi yameongeza haja ya kuimarisha baadhi ya vipengele katika sheria hii," alisema.

Mkuu wa Divisheni ya Watoto wa Idara hiyo, Mohammed Jabir, alisema kipengele namba 18 cha uanzishaji na uendeshaji mahakama ya watoto kimeweka wazi aina ya makosa na muda ambao mshtakiwa atapaswa kutumikia adhabu au kifungo.

Alisema adhabu hiyo si kali na kwamba ni muhimu marekebisho yafanyike katika kipengele hicho.

"Kipengele namba 12 kimezingatia majukumu ya wazazi na jinsi ya kuwasiamia watoto ila bado wazazi hawakielewi na hawakitumii inavyotakiwa kwa ajili ya kuleta mageuzi katika malezi bora," alisema Mohamed.

Hakimu kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, Khamis Rashid Khamis, alisema ni wakati sahihi wa kuweka sheria ambayo itatoa mwongozo wa kushughulikia watoto wenye umri wa chini ya miaka 14 na 16 na kuwa na utaratibu wa kusikiliza kesi zao.



Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abass Ali (kushoto), akizungumza wakati akifungua kikao cha ukusanyaji wa maoni kwa wadau mbalimbali wa kupinga ukatili na udhalilishaji dhidi ya mtoto, kwa ajili ya kuifanyia maboresho Sheria ya Mtoto Namba Sita ya Mwaka 2011, katika Shule ya Kidonge Chekundu Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watiwa mbaroni tuhuma za kukutwa na nyara za serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limewakamata watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali na silaha ambazo zinadaiwa kuzitumia katika uwindaji haramu ndani ya mapori tengefu yaliyoko katika Wilaya ya Manyoni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi Stellah Mutahibirwa, aliwaambia waandishi wa habari jana mjini hapa kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika msako uliofanyika kwa siku 19 kuanzia Oktoba Mosi mwaka huu.

Alisema msako huo unaendeshwa na Jeshi la Polisi katika kuimarisha hali ya usalama mkoani Singida.

Kamanda Stellah aliwataja watuhumiwa hao ambao wote ni wakazi wa Manyoni kuwa ni Bathelomeo Saimon (62), Masanja Mlinga (45) kutoka Kijiji cha Heka, Nicodem Eliud (37), mkazi wa Kijiji cha Chokola na Emmanuel Jack (45), mkazi wa Kijiji cha Meatu.

"Kutokana na uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi tumebaini kuwa watuhumiwa hawa wamekuwa wanajihusisha na uwindaji haramu wa wanyama kinyume cha sheria katika mapori tengefu na kuuza nyara za serikali," alisema.

Pia alisema katika msako waliofanywa kwa kushirikiana na maofisa wa idara ya kupambana na wanyamapori, waliwakamata watuhumiwa wakiwa na kipande cha pembe ya mnyama aina ya faru chenye uzito wa kilo mbili na nusu.

Vilevile, alisema wamekamata silaha aina ya Gobole ambayo haijasajiliwa, vipande 94 vya chuma na chupa mbili za baruti ambazo walikuwa wanazitumia kinyume cha sheria.

Kamanda huyo aliwasihi wananchi kuendelea kusalimisha silaha wanazozimiliki kinyume cha sheria katika muda umaalum uliowekwa na Jeshi la Polisi.

## Wanaotoa huduma za kifedha bila leseni ya BoT faini mil. 20/-

**Na Halima Ikunji,** TABORA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema itawachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kutoza faini ya Sh. milioni 20 wafanyabiashara wanaotoa huduma za kifedha bila ya kuwa na leseni kutoka kwao.

Msimamizi wa BoT Idara ya Huduma Ndogo za Kifedha, Joseph Lubava, alitoa angalizo hilo juzi wakati wa mafunzo kwa watoa huduma za kifedha mkoani Tabora.

Alisema mfanyabiashara atakayebainika kufanya biashara hiyo bila leseni, atatozwa kiasi hicho cha fedha au kifungo cha miaka miwili gerezani.

Lubava alisema Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, kifungu cha 16 (1) na (2) inaelekeza mtu yeyote ambaye anajihusisha na biashara hiyo, anapaswa kufuata mwongozo wa kisheria.

Kuhusu mafunzo hayo, alisema lengo kuu ni kuondoa dhana potofu kuhusu gharama za kuomba leseni kuwa ni kubwa, jambo ambalo si la kweli.

Lubava alisema kwa yeyote atakayekuwa tayari kufanya biashara ndogo ya kukopesha fedha, ni lazima kuwasilisha maombi yao mapema ili kupata leseni kwa kufuata sheria na taratibu ambazo zinatolewa na BoT.

Kiongozi huyo alionya Watanzania kukopa fedha katika taasisi ambazo hazijasajiliwa kisheria, akisisitiza wanapaswa kuziepuka ili kutokumbana na kero za kunyang'anywa vitu ambavyo wanaviweka kama dhamana wakati wa ukopaji.

"Taasisi zote zilizosajiliwa tumezipa mwongozo kuanzia kuandaa fomu ya mkataba, mkataba wa mkopo, gharama zao tumeweza kuzipitia na kujiridhisha," alisema Lubava.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaoendesha huduma hiyo akiwamo, Chacha Mzee, waliiomba BoT nyaraka zao ambazo zinakwenda kwao ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili badala ya Kiingereza kwa kuwa wanashindwa kuzitafsiri.

Alisema wamekuwa wakiingia gharama za kulipa watu ili waweze kuwatafsiria na wakati mwingine kudanganywa kilichomo katika nyaraka hizo kupitia watu wanaowaamini kufanya kazi hiyo.

Asifiwe Edison aliishukuru BoT kwa kutoa mafunzo hayo kwa kuwa mambo mengi alikuwa hayafahamu ikiwamo uendeshaji wa huduma ya mikopo kwa wananchi.

Alisema elimu aliyoipata katika semina hiyo itakuwa ni mwongozo mzuri wa uendeshaji biashara hiyo ya kutoa huduma za mikopo.

HABARI KITAIFA

## Jaji Kiongozi ataka majaji wapya kuharakisha hukumu

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewataka majaji wapya wa Mahakama Kuu ya Tanzania kuharakisha utoaji hukumu ili wananchi wapate haki yao mapema.

Aliagiza hayo juzi wakati akifunga Mafunzo Elekezi ya wiki tatu kwa majaji wapya 20 wa Mahakama Kuu ya Tanzania katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) wilayani Lushoto mkoani Tanga.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Mahakama ya Tanzania na kuendeshwa na IJA. Yalifunguliwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, mnamo Oktoba 2 mwaka huu.

Jaji Siyani alisema Mahakama ya Tanzania haitarajii kuona jaji au hakimu anakaa na hukumu bila kuisoma kwa zaidi ya muda uliowekwa kisheria.

“Msizalishe viporo vya hukumu wala nakala za uamuzi wenu. Dunia inakwenda kasi na watu wanataka haki ipatikane kwa haraka.

“Hatutarajii, hatutarajii, hatutarajii kabisa kuwa jaji au hakimu, akae na hukumu bila kuisoma kwa zaidi ya muda uliowekwa kisheria. Sambamba na kusoma hukumu zenu, toeni nakala zake kwa wadaiwa,” aliagiza Jaji Siyani.

Aliwahimiza majaji hao kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa utamaduni wa sasa wa Mahakama ya Tanzania ni majaji kufanya kazi usiku na mchana ili kumaliza mashauri mapema.

“Ninawaambia kweli, tena bila kupepesa macho, wengi wa majaji wenzenu mnaokwenda kujiunga nao, hawalali. Wanafanya kazi usiku na mchana. Mchana wanasikiliza mashauri na usiku wanaandaa uamuzi.

Jaji asiyeiga utamaduni huu, atatambulika haraka kuwa hachezi ngoma wanayocheza wenzake. Ninyi mkaige utamaduni huu na mtapimwa si tu na mahakama, bali na Watanzania wenyewe,” alionya Jaji Kiongozi.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya washiriki wenzake, Jaji mpya wa Mahakama Kuu, Dk. Evaristo Longopa alisema mafunzo hayo yamewajengea msingi ambao utawasaidia katika kazi yao mpya.

“Tunawashukuru wawezeshaji, wametupa ujuzi na mtazamo kuhusu mambo mbalimbali ambayo yatatusaidia sana katika utendaji wetu wa kazi.

“Tunaamini mafunzo haya yametujengea msingi ambao utamsaidia kila mmoja wetu kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu na kwa ufanisi mkubwa,” alisema Jaji Longopa.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo ambao ni majaji wa Mahakama Kuu, Ntuli Mwakahesya na Dk. Dafina Ndumbaro walibainisha kuwa mafunzo hayo yamewawezesha kuzifahamu taratibu, sheria na utamaduni wa Mahakama ya Tanzania. Waliahidi kuyafanyia kazi kwa haraka maelekezo ya Jaji Kiongozi.

# Majaliwa: Wawekezaji wapewe ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania walioshiriki katika Jukwaa la Tatu la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Italia kutoa ushirikiano kwa wawekezaji na wafanyabiashara waliooneshа nia ya kuwekeza nchini.

Majaliwa pia amesisitiza kuwa serikali imeondoa tozo na urasimu uliokuwapo awali kwa lengo la kurahisisha shughuli za biashara na uwekezaji.

Aliagiza hayo juzi wakati wa hafla ya chakula cha mchana iliyofanyika Palazzo Regione Lombardia, Milan, ikiandaliwa na Ubalozi wa Tanzania Italia kwa kushirikiana na Benki ya NMB.

Hafla hiyo ililenga kuwatambua wafadhili na washiriki wa Jukwaa la Tatu la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Italia.

Katika hafla hiyo, Majaliwa alitoa wito kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi wahakikishe taifa linanufaika kwa kuwa mabalozi wazuri wa kutangaza vivutio vya uwekezaji na kuwashawishi wawekezaji kutoka katika nchi wanazoishi kuja kuwekeza Tanzania.

Majaliwa ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Jukwaa la Kimataifa la Chakula Duniani huko Rome, Italia, aliwasisitiza Watanzania kuheshimu sheria za nchi husika.

Alisema kupitia jukwaa hilo, wafanyabiashara na wawekezaji wengi kutoka Italia wameonesha nia ya kuja Tanzania kwa ajili ya kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwamo ya kilimo.

Hivyo, kiongozi huyo aliwataka viongozi na watendaji wa wizara zinazohusika na masuala ya uwekezaji kuchangamkia fursa hiyo.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwataka wafugaji nchini wakubali kubadilika na kufuga kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kunufaika zaidi na shughuli hiyo.

“Tubadilike tupate manufaa zaidi, ufugaji ni uchumi, ufugaji ni maisha na ufugaji ni kazi, hivyo tubadili mfumo wa ufugaji wetu kwa ajili ya kujiongezea kipato zaidi,” alisisitiza.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Latifa Khamis, alisema mamlaka yao imefaidika kwa kushiriki katika jukwaa hilo.

Alisema sekta zote walizozitangaza zikiwamo za ujenzi na viwanda zimeonesha kufurahiwa na wadau wa uwekezaji, hivyo wamejipanga kupokea wafanyabiashara.

Balozi wa Tanzania huko Italia, Mahmoud Thabit Kombo, aliahidi kuwa ofisi za ubalozi wake katika nchi hiyo zitatoa ushirikiano kwa wafanyabiashara na wawekezaji wote walio tayari kuwekeza na kufanya biashara nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Watanzania walioshiriki katika Jukwaa la Tatu la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania, Italia na Milan juzi. **PICHA: OWM**

# Kiwanda cha kuongeza thamani kuku kienyeji kujengwa Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi ina mpango wa kujenga kiwanda cha kuongeza thamani ya kuku wa kienyeji mkoani hapa ili wasafirishwe wakiwa tayari wameshaongezewa thamani.

Waziri wake, Abdallah Ulega, alibainisha hayo juzi alipozungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara na kueleza kuwa kiwanda hicho kitajengwa katika eneo la



ekari zaidi ya 500 linalomilikiwa na wizara.

“Nimezungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, pale kwenye ekari 500 tunatafuta uwekezaji badala ya kuku kutoka Singida kupakiwa katika malori na kwenda kuchakatwa Dar es Salaam, tuweke uwekezaji hapa wachakatwe ndani ya Singida,” alisema.

Waziri Ulega alisema mifugo hiyo ikianza kuongezwa thamani mkoani humu, kutawafanya vijana na wanawake kupata ajira na kujiongezea kipato kikubwa.

Alisema katika kulipa nguvu suala hili, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imepewa Sh. milioni 330 kufanya utafiti wa kuku wa asili wa Singida kwa lengo la kuongeza uzalishaji wake.

Ufugaji wa kuku ni nyenzo nzuri ya kujipatia kipato katika kaya. Hauhitaji mtaji mkubwa na hauna kazi kubwa kiuendeshaji kwa sababu hujitafutia chakula au nafaka katika mazingira husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hoja za CAG zifanyiwe kazi kunusuru ikolojia, utalii Hifadhi ya Kilimanjaro

**SEKTA** ya utalii inachangia robo ya fedha zote za kigeni na kutoa ajira za moja kwa moja 600,000 na nyinginezo zaidi ya milioni mbili.

Ndani sekta hiyo, mna hifadhi za taifa zilizo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Wakati sekta hiyo inaendelea kuwa tegemeo kwa kuingiza fedha za kigeni na kuchangia Pato la Taifa, uendelevu wa ikolojia na utalii wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro uko shakani kutokana na matukio ya moto yanayoikumba hifadhi hiyo mara kwa mara.

Tukio la hivi karibuni ni la mwezi uliopita, moto ulipozuka tena katika hifadhi hiyo. Ni majira kama hayo mwaka jana moto ulipozuka kwenye Kambi ya Karanga na kuteketeza uoto wa asili wa eneo lenye hekta 34.

Hata inaporejewa kanzidata ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, ina matukio mengine makubwa manne ya moto kwenye eneo hilo la hifadhi yaliyotokea ndani ya miaka mitano kuanzia 2015/16.

Kanzidata hiyo inabainisha kuwa mwaka 2015/16 eneo lililoteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3 na la Oktoba 2020 hekta 22.05, kiini kikuu kikitajwa kuwa uvunaji mbaya wa asali, ujangili na mbinu mbaya za kilimo.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hayuko mbali na kinachoendelea hifadhini Kilimanjaro. Katika ripoti zake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 na 2021/22, CAG ameyaangazia kwa kina matukio ya moto hifadhini huko, akipendekeza hatua nne za kuchukuliwa kuyadhibiti.

Wakati matukio hayo yakijitokeza karibu kila mwaka, mdhibiti anasema amebaini TANAPA halina uwezo wa vifaa na hata maandalizi kukabiliana na majanga ya asili.

Katika ripoti yake, CAG anabainisha kuwa mapitio yake ya ripoti ya matukio ya moto iliyotolewa tarehe 23 Desemba 2020 iliyohusu uchunguzi wa chanzo cha moto kwenye Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, yalibaini hifadhi hiyo ilitumia siku sita kuanzia tarehe 11 hadi 16 Oktoba 2020 kuzuia na kuzima moto huo, ambapo kilomita za mraba 96.07 za eneo la hifadhi ziliteketea.

Ripoti hiyo inabainisha moto uliharibu mandhari ya uoto wa asili wa eneo la Moorland na uliua viumbe hai na kuharibu miundombinu ya mbuga ikiwa pamoja na vibanda 10 vya kitalii vyenye uwezo wa kubeba wageni 80.


Ni moto uliosababisha pia upotevu wa mali zenye thamani ya Sh. milioni 993 na wakati huohuo Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro ikatumia Sh. milioni 221.51 kukabiliana nao. Ilibainika pia katika ukaguzi huo kuwa mlipuko wa moto haukuwa wa kwanza kwenye eneo la hifadhi hiyo kwa kuwa kulikuwa na matukio mengine ya miaka ya 2002, 2004, 2008, 2013 na 2016, ambapo jumla ya hekta 357,565 ziliteketea.

Katika hoja zake, mdhibiti alipendekeza serikali kwa kushirikiana na TANAPA wachukue hatua nne ambazo ni pamoja na kufanya tathmini ya athari za milipuko ya moto na kurejesha miundombinu na uoto wa asili kwenye maeneo yaliyoathiriwa na moto.

Hatua zingine tatu kwa mujibu wa CAG ni: Kutumia satelaiti katika kubaini matukio ya moto; kuanzisha kikosi kazi cha kupambana na majanga ya asili; na kutenga bajeti na kununua vifaa vya kisasa vya kuzima moto ikiwa pamoja na helikopta kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya moto na ambayo itatumika kwa shughuli za doria na uokoaji hifadhini.

Nipashe Jumapili tunakumbusha mamlaka husika kufanyika kazi hoja hizi za mdhibiti. Kutokuwa na vifaa vya kutosha na vya kisasa kunaifanya hifadhi ikose ufanisi wakati wa kukabiliana na majanga ya moto, hivyo kuhatarisha uhifadhi, utalii na uchumi wa nchi kutokana na matukio hayo ya moto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# KKK ya Waziri Silaa izingatiwe, jamii iachane na ujenzi holela

**MAAGIZO** ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kwa wataalamu wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha mipango yote ya kupima viwanja inaendane na miundombinu ya maeneo husika yana manufaa kwa nchi na wananchi.

Silaa anatoa maagizo hayo kwa nyakati tofauti anapozungumza na viongozi na watendaji wa sekta ya ardhi katika ziara zake za kikazi katika mikoa mbalimbali nchini.

Anasisitiza kuwa wataalamu wote wa sekta ya ardhi nchini wanapoandaa mipango ya upimaji viwanja nchini, wahakikishe kuna miundombinu itakayosaidia wananchi wanaouziwa viwanja kupunguza gharama za makazi na maisha yao.

Anasema ili sentensi ya jina la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikamilike, lazima wataalamu wanapopima viwanja, viwanja hivyo viwe na uwezo wa kusaidia huduma za miundombinu kwenye nyumba iliyojengwa pamoja na makazi.

Kwa mujibu wa Silaa, suala hilo lazima liendane na aina ya uendelezaji au ujenzi ili mhusika afahamu kama kiwanja alichochukua atajenga nyumba ya aina gani kama ni ya chini ama ghorofa.

Anafafanua kuwa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) katika kipindi hiki anachohudumu wizara hiyo, mkazo wake mkubwa utakuwa kwa zile K mbili za Kupanga na Kupima na kwamba maeneo yote yanayokwenda kupimwa ardhi, basi wataalamu wasijifungie kama wataalamu wa fani moja na kuwaachia watu vichaka.

Silaa anasema mipango sasa ya kupanga na kupima iende ikahusishe miundombinu ya barabara, maji, umeme, maji taka na mkongo wa mawasiliano ili mtu atakayekabidhiwa kiwanja awe anaweza kuishi.

Anachosema Waziri Silaa kinapaswa kuzingatiwa ili jamii iondokane na ujenzi holela wa makazi ambao umekithiri katika maeneo ingamoishi.

Ujenzi huo umekithiri kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na jamii kutozingatia ushauri wa watalaamu wa miundombinu wakati wa kujenga nyumba, uzio na kugeuka kero kwao yanapotokea majanga.

Pamoja ni ukweli kuwa ujenzi wa makazi ni maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini, KKK anazoagiza Waziri Silaa kwa wataalamu wake wa upimaji ardhi ni bora zikazingatiwa ili kuwe na mpangilio mzuri wa nyumba, barabara na huduma nyingine muhimu katika jamii.

Wananchi pia tunatakiwa kuunga mkono agizo hilo kwa kuwa ni ushahidi usiopingika kuwa maeneo ambayo watu wameanza kuhamia na kujenga makazi ya kudumu pasipokuwapo na miundombinu.

Katika maeneo hayo, kukuwa na shughuli za maendeleo, kilimo, ukataji kuni na uchomaji mkaa bila kuwapo na viongozi tunaowaita wajumbe au mabalozi, bali wananchi wamekuwa wakiishi kwa namna wanavyopanga wenyewe.

Katika mapori hayo, mbali na kukosa huduma muhimu za jamii kama maji, barabara, hospitali, umeme na masoko, wananchi wamekuwa wanaishi kwa ujamaa kwa kusaidiana katika shida na raha, lakini baada ya miji kuanza kukua, kunajitokeza changamoto hizo huku baadhi wakidai ni ufinyu wa ardhi.

Inafahamika kuwa katika maeneo hayo, wananchi wanaitana kwa kufahamiana kwenda kununua mashamba, viwanja na ndipo hapo ujenzi holela wa makazi unapoanza.

Matokeo ya ujenzi huo holela ni kukosekana barabara za moja kwa moja hadi kwenye makazi ya watu, kukosa sehemu za kujenga mifereji ya kupitisha maji hasa wakati wa mvua na kusababisha baadhi ya maeneo kukumbwa na mafuriko kutokana na maji kutuama, magonjwa ya milipuko yanayosababishwa na uchafu na mazalia ya wadudu.

Athari nyingine za ujenzi usio wa mpangilio ni pale yanapotokea majanga kama ya moto, magari ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yanashindwa kupita kwenda kutoa msaada na kusababisha maafa.

Waziri Silaa anastahili pongezi kwa kuliona hilo, hivyo chochonde wataalamu wetu KKK hizo zizingatiwe na wananchi tumuunge mkono ili tuwe na makazi bora yenye kufikika kwa urahisi si tu tunapohitaji usafiri, hata wakati wa majanga.

HABARI/SAFU

# Zahanati ya Polisi yapatiwa vifaa

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

BENKI ya NMB Kanda ya Kusini imetoa vifaa vya kuezekea katika zahanati ya polisi iliyoko mkoani Mtwara vyenye thamani ya Sh. milioni 17.

Vifaa hivyo ambavyo vitamalizia jengo la mama na mtoto katika zahanati hiyo ni pamoja na mabati, mbao, misumari na kofia za mabati.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Faraja Ngingo, alisema changamoto za sekta ya afya nchini ni jambo la msingi kwa Benki ya NMB.

Alisema pamoja na makubwa na mengi yanayofanywa na serikali katika sekta ya afya, lakini NMB kama wadau wanao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizo.

"Tulipopata maombi haya ya kuchangia sekta ya afya tulifarijika na kuamua kutoa mara moja vifaa hivi. Ni moja ya ushiriki wetu katika maendeleo ya jamii, tunao wajibu wa kuhakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika na faida tunayoipata," alisema Faraja.

Mganga Mkuu wa Zahanati ya Polisi, ambaye ni Mkuu wa Kikosi cha Afya mkoani Mtwara, Dk. Stephen Kisaka, alisema zahanati hiyo ni moja kati ya vituo 18 vya kutolea huduma za afya mkoani Mtwara na ni moja kati ya vituo 37 vya Jeshi la Polisi.

Huduma zinazotolewa katika zahanati hiyo ni pamoja na wagonjwa wa nje, mama na mtoto na wenye maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na kwa mwezi huhudumia wagonjwa 2,500 mpaka 3,000 na wenye bima ya afya 800 hadi 1,000.

Vilevile, alisema wanahudumia wagonjwa wa msamaha, wazee na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicodemus Katembo, alisema kuwa kituo hiko ambacho wagonjwa wanaohudumiwa asilimia 80 ni raia, kilianza kwa wazo kutoka kwa askari polisi wenyewe na baadaye wakapata msaada kutoka kwa wadau.

"Tunataka ifikapo mwaka 2025 tuwe na kituo kamili cha afya kwa hiyo msaada huu utarahisisha njia ya kufika katika kituo cha afya kabla ya kufika mwaka 2025," alisema Katembo.

Mmoja wa wagonjwa aliyefika hospitalini huko kupata huduma, Rachel Thobias, alishukuru kwa huduma wanazopewa katika Zahanati ya Polisi, akizitaja ni nzuri, hasa kwa upande wa mama wajawazito, watoto na hata wagonjwa wa nje.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mwanahamisi Mukunda, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwa karibu na wananchi.

"Kama asilimia 80 ya wagonjwa wanaokuja hapa ni raia, maana yake mko karibu nao na mnatoa huduma bora," alipongeza Mkuu wa Wilaya.

# Kilichojificha ufaulu mmomonyoko maadili

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUKOSEKANA kwa elimu ya kujitambua na kujiamini shuleni na mafunzo ya stadi za kazi kumetajwa ni chachu ya kudidimiza vipaji vya wanafunzi na matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya taifa.

Meneja Msaidizi wa Shirika GLAMI (Kilimanjaro), Innocensia Mataba, aliyasema hayo jana mkoani Kilimanjaro na kutoa wito kwa serikali kuangalia namna ya kutoa elimu ya kujitambua kwa wanafunzi kabla ya kwenda chuo kikuu.

Mataba aliyasema hayo katika hafla ya kitaaluma (Carear day) iliyojumuisha shule za sekondari (Kidato cha tano na sita) za Ashira na Mwika.

Alisema katika mradi wao wa KISA, wamebaini asilimia 70 ya wanafunzi shuleni wamefika kwa ajili ya kusoma, lakini wengi wao hawajitambui wanapaswa kuwa nani watakapohitimu.

Alisema wanatarajia kufikia wanafunzi 10,000 ifikapo mwaka 2026. Mpaka sasa wamewafikia wanafunzi 1,235 katika mikoa ya Arusha (458) na Kilimanjaro (777).

"GLAMI kupitia mradi wake wa KISA, umekuja na programu maalum ya kuhakikisha tunatembea katika shule na kuwasaidia wanafunzi waweze kujiamini na kuona wanapaswa kuwa nani wafikapo vyuo vikuu.

"Hawa wanategemea kwenda kuanza maisha ya vyuo vikuu katika fani mbalimbali, wanahitaji kujua fani walizochagua, wanawezaje kuzifikia kwa kujua aina ya matatizo wanayokabiliana nayo?" alihoji.

Mataba alisema wanaleta watu wabobezi katika fani husika ili kuwaongoza na wanaamini hilo litasaidia.

Alisema kuwa vijana wengi ambao humaliza vyuo vikuu na kushindwa kujiajiri au kujitegemea hutokana na kukosekana kwa mwongozo bora wa uchambuzi wa fani.

"Mmomonyoko wa maadili, mimba kabla ya kuhitimu masomo, matatizo yote yanayoletwa na kutokujitambua hayatakuwapo, hivyo serikali iweke programu maalum kwa ajili ya kidato cha tano na sita," alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya washauri walezi wa wanafunzi hao, Eva Ngunge, alisema "Mara nyingi tunapokwenda kutambulisha mradi na kuchagua wanafunzi, tunaangalia utayari wao pamoja na historia ya walipotoka ili tuwabadilishe na waende kubadilisha jamii zao wanakotoka."

Baadhi ya wazazi wa Marangu Mtoni akiwamo, Anastasia Mlay, walisema hilo litachangia kuboresha maisha ya wanafunzi na kujitambua.

Erinesta Shio alisema wazazi walio wengi hawana muda na watoto wao na kuchangia kukosa maadili yatakayowasaidia kujitambua.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Msimchanganye Chifu Hangaya na 'umama' wa Taifa



**Na Joseph Kulangwa**

HIVI karibuni akiwa ziarani mkoani Singida, Chifu Hangaya bila shaka alipata mshtuko, aliposikia kauli ikitoka kwa mmoja wa waliokuwa kwenye moja ya mikutano yake, akitaka apewe hadhi ya Mama wa Taifa.

Huo ulikuwa ushauri tu kutoka kwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Cyprian Hilinti, tena akimtaka Chifu Hangaya aridhie wadhifa huo.

Sababu za Askofu Hilinti ni kwa kuwa Chifu Hangaya ni mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Tanzania, kama ilivyopata kutokea kwa mwanamume wa kwanza kuwa Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere kuitwa Baba wa Taifa.

Kilichomgusa zaidi Dk. Hilinti kutaka daktari mwenzake huyo apewe umama wa Taifa, ni juhudi za kupeleka fedha kufadhili miradi mbalimbali. Akamtaka asiogope kelele za mamba, vibwengo wala vinyamkera, kwani Yesu wa Nazareti yupo, vitashindwa na kulegea.

Askofu Hilinti bwana, eti akahanikiza kuwa Taifa haliwezi kukamilika likiwa na Baba wa Taifa lakini bila Mama wa Taifa, kwa sababu watoto watapata malaria.

Kumbe Askofu Hilinti alikuwa anaona wivu, kwamba kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan alikwenda Kanda ya Ziwa machifu wakampa uchifu na kuitwa Chifu Hangaya, basi wa Kanda ya Kati nao wanataka aitwe Mama wa Taifa.assan H

Alikomelea msumari aliposema kumbe Chifu Hangaya anaowasaidia na hata wanaomtukana, wote 'mazi ga nyanza', kwamba wanamwita mama, hivyo yeye anastahili kuwa mama wa Taifa, yeye ni mama wa wote na upendo wa wote.

Hakika mimi simpingi Askofu Daktari Hilinti kwa mawazo yake haya mujarabu, kwamba Rais Samia kwa haya aliyoyafanya katika kipindi kifupi cha uongozi wake, anastahili jina lolote linaloashiria wema wake.

Anastahili heshima iwayo yote, kutoka kwa kila Mtanzania anayejua fika ni nini maana ya amani, upendo, utulivu, mshikamano na maridhiano, kwa mustakabali mwema wa Taifa.

Hakuna asiyejua mchango wa Chifu Hangaya katika kufikia kuunganisha Watanzania hivi leo walivyo, ikilinganishwa na miaka michache iliyopita, ambapo wengi walikuwa wakitafuta pa kutokea, kujitibu majeraha.

Kwangu mimi hata angeitwa Mama wa Mbingu, wala nisingebisha kabisa, kwa sababu anastahili umama kwa kuwa ni mama, lakini hapa kwa Mama wa Taifa, mmh bado nasita kidogo.

Ninajua Mwalimu Nyerere alipewa jina hilo, kwa mchango wake wakati wa kusaka uhuru wa nchi hii na kujenga katika utulivu, amani na umoja kwa miaka 24 mpaka alipostaafu.

Ukienda India, tulikokuwa hivi karibuni, utasikia majina hayo hayo ya Baba wa Taifa na Mama wa Taifa, kutokana na historia ya Taifa hilo, nenda pia Afrika Kusini, ni hayohayo. Yanahusu hasa mchango wa kihistoria katika kupambania uhuru.

Bahati mbaya sijasikia Chifu Hangaya akikubali au kukataa ushauri wa Daktari mwenzake Hilinti, yawezekana bado amebeba ushauri wa aliyekuwa Askofu Mkuu wa Kanisa hilo hilo, Daktari Fredrick Shoo, aliyemtaka anyamaze kuhusu la DP World na Bandari.

Lakini kuna wakati huko nyuma, watu waliibuka na mapendekezo kama haya ya kuwa na Mama wa Taifa, kura zisizo rasmi zikamwangukia Mama Maria Nyerere mjane wa Mwalimu, lakini matokeo yakaishia hewani.

Siku nyingine pia huko nyuma likaibuka la kuwa na Kaka wa Taifa, kura zisizo rasmi zikamtaka Charles Makongoro, kijana wa mwalimu pia, lakini matokeo nayo yakayeyukia mawinguni. Sasa limekuja hili la Chifu Hangaya. Nalo linaonekana kufuata nyayo za mengine hayo mawili ya awali.

Niseme tu, kwamba Chifu Hangaya anastahili yote hayo, lakini Mama Maria angestahili zaidi kutokana na mchango wake wa kumlea Mwalimu kipindi chote hicho cha kupigania uhuru na hata kutuongoza Watanzania.

Inashangaza siku zote tunaimba nyimbo za yalipo mafanikio ya mwanamume, mwanamke yupo, hatuamini kwamba katika mafanikio ya Mwalimu Nyerere alikuwapo Mama Maria nyuma yake? Tusijisahaulishe Wabongo, ohoooo!

Kama kawaida yetu, tunaweza kukubaliana na dhana hiyo, lakini mbona hatuitendei haki kwa vitendo bayana? Hivi ni wapi tumesikia kumbukumbu yoyote ya Mama Maria zaidi ya mtaa wa vumbi ulioko Kigamboni, Dar es Salaam?

Mbona kila kona ya nchi hii tuna kumbumbuku za mumewe tu tena za kumwaga? Ukienda huku Nyerere, kule JK Nyerere, huku Kambarage, kwingine Julius Nyerere. Zote hizo ni kumbukumbu za Mwalimu, huku mjane wake akiambulia patupu kana kwamba hakuna aliolifanya.

Leo utasikia sijui barabara ya Nyerere, barabara ya Sophia Kawawa, Barabara ya Mfugale, Daraja la Mfugale, Daraja la Kijazi, Soko Kuu la Ndugai na wengine wengi ambao hawawezi kabisa kuenea kwenye viatu vya 'Mama wa Taifa', Mama Maria Nyerere.

Ninaamini Chifu Hangaya anaridhika na anachokipata kutoka kwa wananchi wake anaowaongoza na hana sababu ya kutamani umama wa Taifa, kwa sababu hatajilinganisha na Baba wa Taifa hata kiumri. Labda 'Dada wa Taifa'! Kazi Iendelee!

# ACT: Serikali ilipe fedha za wakulima

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali itoe fedha mara moja kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ili wakulima walipwe fedha zao zote wanazodai.

Waziri Kivuli wa Kilimo, Umwagiliaji na Maendeleo ya Ushirika wa chama hicho, Mtutura Abdallah, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alisema serikali inapaswa kuongeza nguvu ya kununua na kuhifadhi chakula.

"Tunarudia wito wetu kwa serikali kupitia NFRA, kuongeza nguvu ya kununua na kuhifadhi chakula cha kutosha miezi sita ili kuwa na akiba ya chakula kama sehemu ya kujiandaa na majanga," alisema. Alisema serikali inapaswa kuweke mazingira bora kwa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji zaidi, kuendelea kutoa ruzuku katika mbolea na kusimamia usambazaji wake na kuhakikisha usalama wa ardhi kwao kwa kushughulikia migogoro ya ardhi.

Abdallah alisema kuwa kwa muda mrefu sasa wakulima nchini wanalalamikia ucheleweshaji malipo ya fedha za mazao yaliyochukuliwa na NFRA.

Alisema chama chao kimefuatilia kwa karibu mwenendo wa ununuzi wa mazao hayo (mahindi) katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Katavi, Njombe na Mbeya na kubaini kuna ucheleweshaji malipo kwa takribani miezi mitatu.

"Itakumbukwa ACT-Wazalendo tulitoa wito kwa kuitaka serikali kununua na kuhifadhi chakula cha kutosha angalau miezi sita ili kujihakikisha usalama wa chakula na kukabiliana na kasi ya kupaa kwa bei za chakula kwa misimu miwili mfululizo. "Serikali ilichukua wito wetu na kuahidi kuongeza uwezo wa wakala wa kununua chakula kutoka kwa wakulima kiasi cha tani 500,000. Ingawa ilikuwa bajeti kiduchu kutosha kwa miezi miwili, angalau ilitoa matumaini kidogo," alisema.

Waziri Kivuli huyo alisema chama hicho kimesikitishwa kuona utekelezaji wa ahadi hiyo unakwenda kinyume. Badala ya kununua chakula, serikali kupitia NFRA imekwenda kuwakopa wakulima na kuwaacha kwa muda mrefu bila matumaini.


Alisema kitendo cha ucheleweshaji malipo kinaathiri uwezo wa wakulima kujiandaa kwa kilimo katika msimu ujao kwa kuwa hawana fedha za kununua pembejeo za kilimo.

Pia alisema kimeshushа imani ya wakulima kwa serikali na kusababisha kukataa kuuza mazao yao kwa NFRA.

Alisema wafanyabiashara wanatumia mwanya huo kununua kwa bei ndogo na baadaye bei zikipanda mzigo wa mfumuko wa bei za vyakula utakuwa mabegani mwa wananchi wa kawaida.

"Bei zinapanda kwa sababu NFRA hawatakuwa na chakula cha kutosha kukiingiza kwenye mzunguko kukabiliana na makali ya bei. Suala la hifadhi na usalama wa chakula ni muhimu sana kwa usalama na amani ya taifa," alisisitiza.

Aliongeza kuwa licha ya kuzalisha chakula cha kutosha, uwezo wa nchi kuhifadhi chakula ni mdogo kiasi cha kuathiri usambazaji na upatikanaji chakula kwenye maeneo yenye mavuno hafifu.




Mkuu wa Idara ya Rasilimali (Huduma Shirikishi) wa Benki ya NMB, Joseph Ngalawa (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa mmoja wa wanafunzi wanne waliofanya vizuri katika masomo ya Biashara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Tatu Rajab Kikanda (katikati), katika hafla iliyofanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji kukopeshwa bilioni 370/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetia saini mkopo wa Dola za Marekani milioni 150 (Sh. 374.283) zitakazotumika kuwakopesha wateja wakubwa waliowekeza kwenye sekta tofauti za uchumi.

Mkopo huo wa kimataifa (international syndicated term facility) umechukuliwa kwenye soko la kimataifa la fedha ambako Benki ya Intesa Sanpaolo na Benki ya Investec zimeshirikiana kufanikisha mchakato huo uliovutia wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Wakati wa kutia saini mkataba huo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki hii, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mpaka kuupata mkopo huo wa kimataifa, mambo mengi yamezingatiwa ikiwamo kukopesheka kwa benki, uthabiti wa menejimenti ya benki, uendeshaji wake kibiashara na pia tathmini ya uimara na uthabiti wa benki unaofanywa na taasisi mahsusi za kimataifa kama Moody's iliyoipatia benki daraja B1.

"Benki yetu imefanikiwa kupata kiasi kikubwa cha mkopo wa fedha za kigeni kutoka soko la kimataifa. Ni mafanikio yanayodhihirisha imani waliyonayo wawekezaji wa kimataifa kwetu kutokana na mfumo wetu mzuri wa uendeshaji biashara, kukopesheka kwetu na uchumi imara wa nchi yetu Tanzania," alisema Nsekela.

Akieleza mafanikio waliyoyapata, Nsekela alisema benki ilituma maombi ya kupata mkopo wa Dola za Marekani milioni 50, lakini wingi wa wawekezaji waliojitokeza ulivuka malengo kwa asilimia 404 kwa kuwa Dola za Marekani milioni 202 zilipatikana.

Hata hivyo, Nsekela alisema licha ya fedha za ziada kukusanywa, Benki ya CRDB imechukua Dola za Marekani milioni 150 sokoni ambazo ilizieleza ndani ya maombi yake ya awali.

"Katika utaratibu huu wa international syndicated facility, taasisi inayohitaji fedha kama ilivyokuwa kwetu Benki ya CRDB, inawasilisha ombi kwa shirika la fedha la kimataifa linalotambulika ambalo hulifikisha kwa wawekezaji tofauti wanaotaka kuwekeza Afrika.

"Kila mwekezaji kulingana na anavyoitathmini taasisi husika inayoomba mkopo huo, husema yuko tayari kuwekeza kiasi gani kati ya kinachoombwa. Hii ndio maana kiasi kilichokusanywa kilikuwa kikubwa kuliko tulichoomba. Tulieleza kuwa iwapo kiasi kitazidi, uwezo wetu utakuwa ni kuchukua mara tatu ya kiasi tulichoomba," alifafanua Nsekela.

Katika kiasi hicho ambacho Benki ya CRDB imekichukua kutoka wawekezaji wa nje wanaojumuisha kutoka Afrika Kusini, Italia, Mauritius, Misri, Ujerumani, Uingereza na Mashariki ya Mbali, Dola za Marekani milioni 122 zitalipwa ndani ya mwaka mmoja na Dola za Marekani 28 milioni zitarejeshwa ndani ya miaka miwili.

Benki ya CRDB ni taasisi ya kwanza ya fedha nchini kutathminiwa na Moody's na kupewa daraja la juu, hivyo kuwa miongoni mwa benki 10 za biashara ambazo ni rafiki kuwekeza barani Afrika.

Kwenye tathmini yake, kampuni ya Moody's imeipa Benki ya CRDB daraja B1 ambalo ni la juu zaidi kupewa taasisi ya fedha kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwenye mkutano huo, Mkuu wa Masuluhisho ya Mikopo kwa Afrika wa Benki ya Investec, Leanne Large alisema "wingi wa wawekezaji waliovutiwa kuwekeza fedha zao katika Benki ya CRDB unadhihirisha kukua na kuimarika kwa benki hii pamoja na ushawishi wake katika uchumi wa Tanzania. Benki ya CRDB inakopesheka zaidi na wawekezaji wengi wanaiamini kufanya nayo biashara."

Mkurugenzi wa Mikopo ya Pamoja wa Benki ya Intesa Sanpaolo, Gustaaf Eerenstein alisema ukuaji mzuri wa Benki ya CRDB tangu ilipoanzishwa mwaka 1996 unawavutia wawekezaji kuiamini kwa kuwa imekuza mizania yake mpaka kufika thamani ya Sh. trilioni 12.5 sawa na Dola za Marekani bilioni 4.9.

"Mkopo huu unadhihirisha ubora wa menejimenti na wafanyakazi wa Benki ya CRDB katika mazingira haya magumu ya biashara tuliyonayo duniani kote ambako biashara nyingi zinayumba kutokana na sababu mbalimbali. Tuna furaha kubwa kuwa sehemu ya wabia wa taasisi hii kubwa ya fedha barani Afrika," alisema Eerenstein.

Baada ya kutia saini mkopo huo, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa alisema fedha zipo, hivyo kuwakaribisha wafanyabiashara wakubwa hasa wanaohitaji fedha za kigeni kuitumia fursa hii kuimarisha miradi yao na kuchangia kukuza uchumi wa taifa.

# Bosi GGML aongoza matembezi kuhamasisha ustawi afya ya akili

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAKATI Tanzania ikiungana na dunia mwezi huu wa Oktoba kuadhimisha uhamasishaji wa afya ya akili, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Terry Strong, ameongoza wafanyakazi na makandarasi wa kampuni hiyo kufanya matembezi ya afya ndani ya eneo la mgodi huo.

GGML imechukua hatua hiyo muhimu katika kipindi hiki cha maadhimisho hayo ili kuikumbusha jamii umuhimu kufanya mazoezi kwa ustawi wa afya ya akili.

Wakiongozwa na Strong, zaidi ya wafanyakazi 30 wa GGML na makandarasi walishiriki katika matembezi hayo yaliyochukua umbali wa kilomita tano kuzunguka eneo la mgodi huo wa mkoani Geita.

Mkurugenzi huyo alisema matembezi hayo yalikuwa njia ya kuufurahisha na kuuchangamsha mwili, kuboresha uhusiano wa kijamii na ustawi wa kiakili miongoni mwa wafanyakazi na kukuza urafiki.

Aliongeza kuwa AngloGold Ashanti - GGML imekuwa inazingatia kipaumbele cha ustawi wa kiafya wa wafanyakazi wake.

Alisema: "Mwezi huu tunapofanya matembezi haya kuamsha ari mpya ya ufanyaji mazoezi mahali pa kazi, hii inadhihirisha kuwa ndani ya GGML kila mtu anathaminiwa, anajishughulisha na ana uwezo wa kiakili, tunajivunia kushiriki katika maadhimisho haya ya kimataifa na kuunga mkono ustawi wa afya ya akili kwa wafanyakazi wetu.

"Afya ya akili inaathiri watu wengi; ni suala muhimu sana na nina furaha kuwa hapa kuliunga mkono kupitia maadhimisho haya. Ninawatakia ninyi nyote na familia zenu heri na kuwatia moyo katika kuzingatia suala la kuangalia afya yako ya akili.

"GGML tunaamini kuwa wafanyakazi wenye afya bora na wanaojishughulisha ni muhimu kwa mafanikio yetu kama kampuni inayojishughulisha na uchimbaji madini. Tunathamini kila mfanyakazi aliye katika timu yetu na tumejitolea kuhakikisha anakuwa katika mazingira bora kwenye nyanja zote."

# MAISHA

OKTOBA 22, 2023
Nipashe

Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*




Ukurasa 13

**'Sweatpants' inaongeza furaha kwenye bata la jioni**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Siri ya nyumba imara iko hapa



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Epuka uzee fuata njia hizi...

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| B | ■ | S | H | I | B | A |
| W | ■ | ■ | ■ | K | ■ | M |
| A | ■ | K | W | A | ■ | I |
| W | A | O | ■ | T | I | N |
| A | ■ | N | A | E | ■ | I |
| N | ■ | D | ■ | ■ | ■ | K |
| I | M | A | N | I | ■ | A |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MTU, MBU, AGA, PAO, OBAMA, KIUNO, MAMBA, UPUPU, ONDOSHA, MAKALIO

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI. JE, KAMBA IPI IMESHIKA SAMAKI?






Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa na wenzake wakicheza nje ya nyumba yao wakati manyunyu ya mvua yakianguka. Mama yake alitoka ndani haraka kwa ajili ya kumkataza.

Mama: Mwanangu ondoka hapo huoni mvua inaanza kunyesha?

Juma: Mama mbona hakuna mvua, haya ni manyunyu tu.

Mama: Hata kama ni ndogo haupaswi kukaa hapo

Juma: Mbona mwalimu wetu alituambia kwamba ndondondo si chururu, yaani sitalowa mama.

Mama: Mwalimu wako alimaanisha kwamba kila kitu ufanye kwa kiasi na si kama ulivyoelewa wewe.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mke akimbia familia, aishi klabu za usiku

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya Maisha Yalivyo. Bado tunaangaza vituko vya baadhi ya wanawake waliobahatika kuwa na ndoa nzuri, lakini shubiri inazitafuna kwa njia mbalimbali.***

Vipo visa vingine ukivisikia, utavifananisha na mchezo wa kuigiza, kumbe ni kweli. Kumbuka kituko katika mada mbili zilizopita, mama kaolewa anazaa na mumewe ndani na pia anamchomekea mume huyu watoto anaozaa na mwanamume mchepuko!

Shetani anamfuatilia sana mwanamke, lengo likiwa kumtoa katika nafasi yake ya kuijenga familia iliyo bora.

Na anachofanya anasubiri mwanamke apige hatua kubwa ya mafanikio ndipo anamvuruga kumharibia.

Hebu sikia kituko hiki. Yupo mama mmoja ameikimbia ndoa yake kule Tabora akatinga jijini Dar es Salaam kusaka maisha. Cha ajabu ameishia katika vilabu vya starehe usiku. Si kwamba alikuwa na maisha duni, la hasha.

Ameolewa, mume mfanyabiashara mkubwa pale mjini Tabora, ana watoto watatu wapo shuleni. Pale Tabora mama alikuwa na mjasiriamali. Hakuwahi kugombana na mumewe iwe eti sababu ya kuiacha familia yake.

Hivi karibuni mama huyu akakutana na bango lililokuwa likitangaza kongamano la kidini jijini Dar es Salaam, kuhusu kufichua matatizo yaliyojificha yanayotesa maisha ya watu. Akafuatilia maelekezo na kufika kwenye mkutano huo.

Baada ya kufika, mama huyu alikuwa miongoni mwa watu wengi waliofichuliwa matatizo yao. Alipofunguliwa ufahamu akaeleza nini kilichotokea katika maisha yake hata kujikuta yupo Dar ambako hana ndugu na maskani yake yalikuwa katika klabu za starehe za usiku.

Akitoa ushuhuda wake mwenyewe akasema hivi;- “Mimi ni mke wa ndoa ya miaka tisa, nina watoto watatu. Tunapendana na mume wangu. Ni mwenyeji wa Tabora na nilikuwa na shughuli zangu za ujasiramali.

“Lakini cha ajabu siku moja nilijikuta ninasikia sauti ikiniambia niondoke nyumbani niende Dar es Salaam. Sauti hii ilikuwa na nguvu sana. Ndipo nikavizia mume wangu hayupo nikaandaa begi, nilitaka tu kwanza nifike Dar ndipo nitoe taarifa kwake.

“Kufika Dar, mume akanipigia simu mke wangu uko wapi? Nikamjibu nimeshaondoka nipo Dar kusaka maisha. Mume alishangaa, lakini nikamwambia ndio hivyo, wewe niache.

“Dar sikuwa na mtu nimjuaye ila nilitafuta penye klabu ya usiku na nilipopata ndipo palikuwa maskani yangu. Nilijitahidi kujichanganya na niliowakuta, maisha yakaendelea.

“Nikapata marafiki wa kuambatana nao, ni kulewa na kubadilisha wanaume bila kuchoka. Mume wangu alikuwa akinitumia ujumbe kunisalimia na kunisihi nirudi nyumbani, watoto pia wananiulizia, lakini bado sikubadili msimamo.

“Cha ajabu kila mwezi alinitumia Sh. 300,000 za matumizi miezi sita ya utoro. Sasa nimeokoka, nimefunguliwa, ninajiandaa kurudi Tabora kwa mume wangu!”

Kituko hiki kinanikumbusha mama mmoja alitimka na kuiacha ndoa yake baada ya kumlazimisha mume wake aache kazi ya kuongoza watalii, vinginevyo ataondoka kwao. Tayari walishazaa mtoto mmoja.

Sababu ni wivu akihisi kuwa mumewe ana mwanamke mwingine. Hata akisikia anaongea na mfanyakazi mwenzake wa kike anahisi ni hawara.

Mume alipokataa ushauri huo, siku moja bibie alifungasha na kumchukua mwanawe, kisha kutimkia kwao. Pamoja na mume kumfuatilia alikataa kurudi.

Lakini cha ajabu baada ya muda kupita mume alipomfuatilia akagundua kuwa alishaolewa na kuzaa na mtu mwingine na sasa ni mkulima kwani mume huyo ni yule anayefanya vibarua kwenye mashamba ya watu. Unatoka pazuri unaangukia pabaya. Ama kweli mkataa pema pabaya panamwita!

Wapo watu wa aina hii lakini binafsi nikiamini kuwa si utashi wao bali msukumo toka anga za giza zinazoua hatma ya mtu.

Niishie kusema tu kwamba pengine ni ufinyu wa fikra unaotokana na malezi/makuzi au tabia ya ujinga isiyotaka mabadiliko katika maisha yanayotuzunguka.

Mpenzi msomaji, wapo kinamama ambao sijui ni madudu gani huwaingia akilini na kutifukatifuka hata kufikia kuchukua uamuzi unaowapeleka kusiko.

Angalia bibie huyo, kwa maelezo ya mumewe inaonesha hakuwa na matatizo naye kwa maana ya matunzo kwani alifanya kila awezalo kuona maisha yao yanakuwa bora zaidi.

Na hata mama huyo wa Tabora mume hakuna na tatizo naye. Hadi leo anataka arudi. Je, una maoni au kisa cha maisha? Ujumbe mfupi 0715268581.

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Pumzika kujitwika majukumu yasiyo yako

UNABEBA majukumu ya watu ili iweje? Unadhani unamfurahisha nani? Una matumizi ya ovyo. Ni zaidi ya kufuru.

Ndiyo unachukulia matatizo ya watu kama vile ni yako, na unajipa wajibu wa kuyasuluhisha ili uteke heshima ya ukoo au jamii inayokuzunguka.

Ndugu wakikwama, unajitwisha mzigo wa matatizo, marafiki wakikwama unabeba matatizo yao na kila mtu vivyo hivyo.

Hapa, sizungumzii kusaidia, hapana! Bali ile namna ambavyo unafanya mambo kama vile ni yako.

Baada ya muda unajikuta una majukumu mengi kuliko uwezo wako, uchumi wako. Mara mtoto wa kaka yako, dada yako, mjomba au shangazi, umejipa kazi ya kutatua hali yake ya kimaisha.

Umejiachia kama hukumbuki kuna maisha yako na familia yako unatakiwa uyatengeneze mapema.

Kila iitwapo kesho, hukosi jambo, sijui nani? Na kila mtu anakuangalia wewe. Eti unatafuta heshima kwenye familia, ukoo na hata jamii inayokuzunguka.

Kinachotokea ni kuwa wewe unayachukua yale majukumu, yanakuwa yako na yanakuwa ndiyo malengo yako, kuwasaidia wahusika kuyatatua.

Lakini wale ambao unawasaidia nao wanalemaa, kwa kuwa upo, wanazilazimisha akili zao, kuamini kuwa si msaada bali ni majukumu yako.

Wanakuwa wavivu na kuacha kutimiza wajibu wao wakijua upo. Wakati mwingine hata ukikosa wanalaumu kana kwamba ni wajibu wako.

Kama una tabia hizi, jitathmini mara tatu na uchukue uamuzi mgumu.

Ni muhimu kuanza kubadilika. Anza kwa kutambua tatizo lako, weka malengo yako ya kimaisha.

Kuwa na malengo, kutakuzuia kufanya mambo mengine yote haya ya kukumalizia fedha.

Hebu acha huo ulimbukeni. Kwa sababu hali hiyo itakufanya kuwa na nidhamu ya fedha na kuzitumia kutokana na malengo uliyojiwekea.

Waingereza wanasemaga ‘It is your time now to stand alone’ (Ni muda wako wa kusimama peke yako).

Yaani una matumizi ya ovyo kama nini. Ndiyo unanunua vitu vya ovyo, kwa kuwa huna malengo kwamba hujapanga ‘nikipata fedha nazipeleka wapi?’ Unajikuta unakuwa na fedha nyingi ambazo ni taslimu kila siku.

Kisaikolojia unajiona kama una fedha nyingi, unajikuta unanunua vitu ambavyo hata ulikuwa huvihitaji.

Mwisho wa mwaka 2023 unakaribia, siku hazigandi. Huna ulilolifanya zaidi ya anasa na shughuli mbili tatu za kuchangia harusi za watu badala ya elimu.

Wanao nyumbani, hata mmoja wao hawasomi shule za mchepuo wa Kiingereza, wako shule za umma, ila wewe ni bingwa wa kuahidi na kutoa michango ya shughuli mtaani.

Kiufupi, uko kama ulivyo. Unajifariji maisha ni yale yale, acha ule bata, lakini unasahau kuna mzigo mwingine umejitwika wa familia tegemezi.

Haya! Sehemu ya kutembea, unapanda bajaji, unapanda bodaboda, kwa kuwa una Sh. 1,000 ipo mfuko wa shati.

Umeshiba lakini una 200/- unanunua karanga. Likipita chungwa, kashata, nipe na kahawa.

Huhitaji shati, lakini una 100,000/- mfukoni na huna pa kuipeleka. Basi unaamua zako kununua vitu vingi ambavyo hata huvihitaji.

Fedha zako zinakwenda huko, lakini ungekuwa na malengo, ungezipeleka kwenye malengo yako na si kununua hivyo.

Woh! Hujifunzi tu kuacha kutoa zaidi kuliko uwezo wako? Hivi unakwama wapi wewe?

Kama wewe ni yule mtu ambaye kila mtu akipata shida, basi mtu wa kwanza kukufikiria ni wewe basi una tatizo.

Inawezekana unaona ni jambo jema na ni kweli kiubinadamu ni jambo jema, lakini kiuchumi ni kuwa unawafanyia kazi wengine.

Yamkini hata huwapi msaada, wanakopa. Lakini jua kwamba wao hukopa kufanyia mambo yao. Ina maana wakati huo wewe hufanyi ya kwako.

Unakuwa kama benki au taasisi ndogo za fedha kama SACCOS, VICOBA na hizi wanaita taasisi za kausha damu, lakini unawapa pesa bila kutoza riba.

Kwamba wewe huna kazi ya kuzifanyia pesa zako. Kwahiyo, unawapa wakazizalishie wao.

Rafiki yangu, pumzika kujitwika majukumu yasiyo yako, unazika talanta yako. Achana na haya mambo, iko siku utanikumbuka kwa hili andiko.


***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.***

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***


***Simu: +255 767 535490***

# HARUSI





Je, unataka kufunga ndoa na unahitaji kuwa tofauti? Unaweza kuchagua matoleo haya mapya ya magauni kama inavyoonekana pichani. PICHA: PINTEREST







# MITINDO

# ‘Sweatpants’ inaongeza furaha kwenye bata la jioni



KAMA wewe ni mpenzi wa mitindo ya kisasa, tayari umefahamu ustadi wa kuvaa nguo aina ya leggings kwenye hafla rasmi iliyosheheni kila aina ya furaha.

Leggings ni nguo inayobana sawa na ile ya mazoezi ndio msingi katika mavazi yanayovaliwa katika sehemu tulivu na zenye misisimko.

Hata hivyo, unaweza kuvaa vazi lingine na ukapendeza wakati wa sherehe zinazoandaliwa nyakati za likizo.

Jibu ni ndiyo, hakuna vazi lingine bali ni Sweatpants.

Siri kubwa ni kuchagua aina nzuri ya nguo yako na kupata jozi iliyokamilika ya Sweatpants.

Hakuna shaka unapotoka na kwenda kufurahia maisha, mwili wako hautatawaliwa na jasho kwani nguo hizo zinatosha kukupa ukavu wakati wote.

Utakapokuwa eneo husika utajihisi uko sehemu bora zaidi, sio tu kwa mwonekano unaovutia bali kwa ulinzi imara wa vazi ulilotumia.

Ili kuongeza mvuto zaidi unashauriwa kuongeza vitu vingine vya thamani kama mkufu, saa na kiatu maridadi.





UREMBO



## EPUKA UZEE

# Fuata njia hizi...

WIKI iliyopita safu ya urembo ilieleza namna unavyoweza kuondoa makovu ya uzee kwa kutumia vitu vya asili ukiwa nyumbani kwako.

Makovu ya uzee mara nyingi hujulikana kama liver spots au sun spots na huwa ni doa jekundu au hudhurungi kwenye ngozi, ambalo kwa kawaida hutokea kwenye uso, mikono na shingo.

Katika kesi nyingi, madoa haya huwa yanaongezeka kutokana na miale ya jua.

Tunaendelea na tiba muhimu za nyumbani za kupunguza makovu ya uzee.

**Juisi ya ndimu**

Tiba nyingine nzuri ya nyumbani ni kutumia juisi ya ndimu kupunguza makovu ya uzee, madoa na kasoro za ngozi.

Chukua juisi ya ndimu na upake moja kwa moja kwenye makovu ya uzee.

Ikiwa juisi ni kali sana, unaweza kuichanganya na maziwa ya mtindi na kisha kuipaka kwenye uso.

Mtindi utaacha ngozi yako laini na juisi ya ndimu itasaidia kufifisha makovu ya uzee.

Fanya zoezi hili kila siku kwa wiki mbili mpaka mwezi kupata matokeo mazuri.

**Mafuta ya Mbono (Castor Oil)**

Inaaminika kuwa mafuta ya mbono ni tiba muhimu ya nyumbani ya kupunguza makovu ya uzee.

Paka mafuta ya mbono kwenye makovu ya uzee kwenye uso na shingo kila siku asubuhi na jioni baada ya kuoga ili upate matokeo mazuri.

**Angalizo**

Endapo umeshaanza tiba ya hospitali usikatishe. Lengo siyo kukufanya uache matibabu kutoka kwa daktari wako, bali ni kukusaidia upate nafuu wakati unajiandaa kwenda hospitali.

Kama njia zote hizi hazijakupa matokeo mazuri, tafadhali nenda hospitali mapema na muone daktari.

Yawezekana kuna tatizo kubwa kiafya linalohitaji uangalizi wa karibu na vipimo zaidi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Chapati za maji

KATIKA safu yetu ya mapishi tunaelezea namna ya kupika chapati za kumimina, au kama zivyozoeleka kwa jina la chapati za maji.

Chapati za aina hii zimezoeleka kupikwa kwa kutumia maji lakini, leo tunaelekezana namna ya kuzipika kwa kutumia maziwa.

**Mahitaji**

Unga wa ngano nusu kilo na mayai 4, maziwa ya kutosha, chumvi kijiko cha chakula, tangawizi ya unga kijiko kimoja cha chai, vitunguu maji, hoho, karoti na mafuta.

**Namna ya kuandaa**

Changanya unga, tangawizi pamoja na chumvi au sukari kwa wale wanaopenda kuweka sukari kwenye chapati za kumimina.

Sugua vitunguu maji kama unavyo sugua karoti upate vijiko viwili vya chakula au kata vipande vidogo vidogo, andaa mayai katika bakuli lingine uyakoroge.

Anza kuchanganya mchanganyiko wako wote wa mayai, karoti, hoho, vitunguu na maziwa kwenye unga ulioandaa uku ukikoroga hadi pate mchanganyiko laini.

Weka kikaangio kwenye moto, weka mafuta kidogo na yapashe moto chota mchanganyiko kijiko kikubwa, tandaza vizuri kwenye kikaangio, acha iive mpaka inapata rangi ya kahawia. Geuza upande wa pili na kuongeza mafuta kidogo uku ukiendelea kuigeuza na hapo zitakuwa tayari.

Chakula hiki unaweza kula jioni au usiku, unaweza kula kwa supu au mchuzi wa nyama au samaki. Pia unaweza kula kwa kushushia na chai, soda, juisi au maji.



MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

## Tengeneza kimsitu chako nyumbani

WATAALAMU wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa uwepo wa miti mbalimbali nyumbani unaweza kutengeneza madhari mujarabu ya kukuongezea utulivu na kuondoa msongo wa mawazo uwapo nyumbani.

Wanaeleza kuwa ni suala la kuamua na kuanza kutengeneza madhari hiyo ya kuvutia kwa kupanda miti tofauti tofauti, mikubwa kwa midogo ili kupata msitu unaoutaka.

Mtaalamu Bahati Boaz, anasema iko miti isiyokua haraka inayoweza kupandwa kwenye makopo makubwa ya maua na kuwekwa kibarazani au chini kwa mpangilio unaoutaka.

Anasema ipo inayostawi vizuri kama ikipata kivuli na ipo inayohitaji jua na mwanga zaidi; na kushauri kuwa kabla ya kuanza kutengeneza msitu nyumbani kwako, fahamu vyema miti na maua unayoihitaji.

Anapendekeza kuwa miti mizuri ni ya matunda kama michungwa, miembe na minazi kulingana na ukubwa wa eneo lako, kwa kuwa inaweza kuwa na faida zaidi, lakini miti mingine nayo inahitajika ili kukamilisha dhumuni la kuwa na mazingira ya asili nyumbani.

Anasema tafiti nyingi zimethibitisha namna ambavyo miti inaweza kusafisha hewa japokuwa ni muhimu kuzingatia kupanda ile isiyohatarisha nyumba au kuvuta wadudu wakali kama ng'e, tandu na nyoka.

Baadhi ya miti inayopendekezwa kupandwa ni parlor palm unaotajwa kusafisha sana hewa na wenye uwezo wa kutengeneza msitu haraka.

Mwingine ni yucca cane ambao unaweza kuupanda karibu na mti mwingine kwa kuwa unastawi vizuri ukiwa kwenye kivuli, japokuwa hauhitaji maji mengi.

Anashauri kwamba chini ya miti kupandwe maua ili kutengeneza mazingira asilia.





# Siri ya nyumba imara iko hapa

UIMARA wa nyumba ni kuhimili mambo mengi ikiwamo changamoto zinazojitokeza katika nyakati za mvua, upepo mkali na uzito wowote unaoipiga.

Peter Akoye anajishughulisha na masuala ya ujenzi wa nyumba. Anasema uimara na uzuri wa nyumba unategemea vitu vingi.

Kwamba kwa nyumba za kawaida, uimara wake huanzia kwenye ujenzi wa msingi, kuta, paa, nguzo, mihilimi, milango, madirisha na dari. Yote haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa ujenzi wake.

"Nyumba imara na mwonekano mzuri ni alama kwa eneo husika, huongeza thamani ya jengo, mandhari ya jengo iliyowekwa katika uzuri, hata huleta hisia na utulivu, furaha na uchangamfu kwenye familia na mtaa.

"Ni muhimu jengo liwe imara na uzuri unaoendana na matumizi yake, kama ni kwa ajili ya biashara, basi liwe lenye mvuto unaovutia hata wateja, kama ni kwa ajili ya kuishi familia, basi ichangie kuleta amani na furaha nyumbani," anasema.

Akoye anashauri kwamba ni vyema nyumba ikafanyiwa usanifu mzuri na bora kuanzia jengo lenyewe, mazingira ya ndani, madhari ya nje ili yabebe maana fulani na kwamba ni muhimu kuwa makini na maana hiyo unayomwambia mtu kupitia nyumba yako.





"Rangi, mpangilio, mpishano, kimo, ukubwa, umbile la nyumba yako huathiri hisia za mtumiaji. Pia niwakumbushe kwamba rangi nyeupe kwenye nyumba huleta hisia za usafi, utaratibu na amani.


"Kijani huleta hisia za utulivu, uasili. Nyekundu huleta hisia za kusisimua, shauku, changamfu. Rangi ya waridi huleta hisia ya furaha na ya buluu huleta hisia za uasilia na utulivu pia.

"Kwa hiyo, ni muhimu kufanya chaguo sahihi unapopanga au unapokamilisha ujenzi wa nyumba ya ndoto yako," anafafanua.

Anashauri kwamba jambo la msingi ni kujenga nyumba unayohitaji, itakayokidhi mahitaji ya sasa na baadaye, yenye usalama na uimara, iliyo katika uzuri wake na kuepuka kujenga usiyoihitaji.

Kufahamu aina ya nyumba inayokufaa kujenga ni miongoni mwa mambo yanayosisitizwa na mtaalamu huyu kwa kuwa ndiye mahali muhimu ambapo kila mtu anapatia faraja na kupata muda wa kupumzika baada ya shughuli nyingi za kujitafutia kipato.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

...SIO NGUO TU, HATA SAMAKI ANAVULIWA...



Malori ya msaada yakivuka mpaka wa Rafah kwa mara ya kwanza kuingia ndani ya ukanda wa Gaza jana PICHA: AFP

# Malori ya misaada yaingia Gaza, Hamas yawaachia mateka wawili

**TEL AVIV,** Israel

MALORI 20 yaliyobeba msaada wa kiutu yameingia kwa mara ya kwanza ndani ya ukanda wa Gaza jana kupitia mpaka wa Rafah uliopo upande wa Misri.

Mashirika kadhaa ya habari yameripoti taarifa hizo kupitia waandishi wa habari walioko upande wa Misri na ukanda wa Gaza.

Mkuu wa Misaada ya Kiutu wa Umoja wa Mataifa, Martin Griffiths, alisema ana matumaini kuwa shehena hiyo itakuwa ni mwanzo wa juhudi endelevu za kupeleka mahitaji muhimu kwa watu wa Gaza.

Pia alitahadharisha kwamba msafara huo wa kwanza haupaswi kuwa wa mwisho.

Hata hivyo, taarifa zilieleza kwamba baada ya malori hayo kufanikiwa kuingia upande wa pili, mpaka huo umefungwa tena.

Msafara huo uliobeba msaada wa kiutu unasimamiwa na Shirika la Hilali Nyekundu la nchini Misri, ambalo ndiyo lina jukumu la kuratibu zoezi la kupelekea misaada ya Umoja wa Mataifa.

Shehena hiyo ni ya kwanza tangu kuzuka kwa vita wiki mbili zilizopita kati ya Israel na kundi la Hamas.

Msaada wa waanza kuingia baada ya shinikizo la kuwanusuru watu milioni 2.4 wanaoishi ukanda wa Gaza.

Kivuko cha Rafah ndiyo njia pekee ya kuingia Gaza ambacho hakiko chini ya udhibiti wa Israel, ambayo iliruhusu kuingizwa kwa msaada wa kiutu kutokea Misri baada ya ombi kutoka Marekani.

Israel inaendelea kuishambulia Gaza kwa makombora tangu kundi la Hamas lilipofanya shambulizi kubwa katika historia ya miaka ya karibuni ndani ya ardhi ya Israel.

Shambulizi hilo la Oktoba 7 lilisababisha vifo vya karibu watu 1,400 nchini Israel na mamia wengine kuchukuliwa mateka.

Tangu wakati huo Israel imeweka vizuizi vikali zaidi kwa eneo la ukanda wa Gaza ikisitisha usambazaji wa chakula, maji, dawa na nishati ya umeme pamoja na mafuta.

Israel ilisema inataka kulitokomeza kundi la Hamas inaloonekana kama la kigaidi.

Viongozi kadhaa duniani wameikaribisha hatua ya kuanza kuingia msaada Gaza.

Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, alisema hatua hiyo muhimu ya kupunguza madhila kwa watu wasio na hatia.

Kansela Olaf Scholz wa Ujerumani amesifu taarifa za kuwasili kwa msaada wa kiutu Ukanda wa Gaza akisema ni habari njema na kwamba Ujerumani itafanya kazi kupitia njia zote kuondoa mateso yaliyosababishwa na mzozo huu.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Uingereza, James Cleverly, alisema kuwasili kwa msaada Gaza hakupaswi kuwa jambo la mara moja na badala yake malori zaidi lazima yaruhusiwe kwa siku zinazokuja.

MATEKA WAACHIWA

Kundi la Hamas limewaachia huru mateka wawili raia wa Marekani, Judith na Natalie Raanan wameachiliwa huru na kundi la Hamas.

Taarifa kutoka ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel ilithibitisha kwamba mateka wawili wa Marekani, Judith Raanan na binti yake Natalie, waliachiliwa kutoka mikononi mwa kundi la Hamas jana.

Taarifa hiyo inaongeza kuwa Brigedia Jenerali Gal Hirsch na vikosi vingine vya usalama waliwapokea watu hao kwenye mpaka wa Ukanda wa Gaza.

Rais wa Marekani, Joe Biden, ametoa taarifa kujibu kuachiliwa kwa mateka hao akisema anafuraha na kwamba hivi karibuni wataunganishwa tena na familia yao.


Alisema raia hao wa Marekani waliooshikiliwa na Hamas tangu Oktoba 7, wamevumilia majaribu mabaya kwa siku 14.

Biden alizishukuru serikali zote mbili za Qatar na Israel kwa kufanya kazi pamoja ili kuwezesha kuwaachiliwa huru na alisema serikali yake inafanya kazi mchana na usiku kuwakomboa raia wengine wa Marekani waliotekwa na Hamas.

Siku sita baada ya Hamas na wanamgambo wengine kuvamia eneo la kusini mwa Israel, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, alikutana na kiongozi wa nchi ya Qatar kujadiliana kuhusu hali ya mateka waliopelekwa Gaza.

Qatar ilijitolea kutumia ushawishi wake na Hamas kusaidia kuachiliwa kwa mateka hao.

Siku za mazungumzo nyeti zilifuata na wapatanishi wa Qatar wakizungumza na Hamas na Waisrael, ingawa hakuna ubalozi wa Israeli nchini Qatar. **DW**



Mateka wawili wa Marekani, Judith na binti yake Natalie Raanan waliachiliwa huru na kundi la Hamas jana.

# Wanasheria wamtetea Bazoum

**NISAMEY,** Niger

UTAWALA wa kijeshi nchini Niger ulitangaza kuwa rais aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum alijaribu kutoroka pamoja na familia yake.

Hata hivyo, wanasheria wa rais huyo aliyeondolewa madarakani walikanusha madai hayo wakieleza yamepikwa na uongozi wa kijeshi.

Wakati huo huo, Ufaransa ilisema vikosi vyake vitakamilisha hatua ya kuondoka nchini humo kufikia mwishoni mwa mwaka huu kama ilivyopangwa.

Alhamisi jioni, utawala huo wa kijeshi ulisema kuwa una-wasiwasi-juu-ya-hatima-ya-rais-aliyependuliwa Niger Bazoum alijaribu kutoroka pamoja na familia yake, wapishi wawili na maofisa wawili wa usalama.

Katika taarifa kupitia televisheni ya taifa, msemaji wa utawala huo wa kijeshi Amadou Abdramane, alisema kuwa mpango huo wa kutoroka ulihusisha kuingia mafichoni viungani mwa mji mkuu Niamey kabla ya kusafiri kwa helikopta za taifa moja la kigeni lenye nguvu kueleka Nigeria.



Kundi la mawakili wanaomtetea Bazoum ambaye yuko chini ya kizuizi cha nyumbani tangu alipoondolewa kwa nguvu madarakani mnamo mwezi Julai, walisema taarifa hizo sio za kweli na yametungwa dhidi ya kiongozi huyo.

**Hata hivyo, wanasheria wa rais huyo aliyeondolewa madarakani walikanusha madai hayo wakieleza yamepikwa na uongozi wa kijeshi.**

# Raia wa India kizimbani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

RAIA watatu wa India wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga kujibu mashtaka ya uhujumu uchumi na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 75.5.

Washtakiwa hao, Kerai Dervaj Khmji, maarufu Babu Jii, Nehal Mehta na Jaydeep Kumar Parekh, wanadaiwa kutenda makosa hayo wakati wakiendesha kampuni ya ununuzi madini ya dhahabu ya Nadoyo Minerals Trade Company.

Mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Edimund Kante, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Yamiko Mlekano, alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza, Khmji anakabiliwa na shtaka la kuongoza genge la uhalifu na kufanya biashara ya madini kinyume cha sheria.

Mlekamo aliendelea kudai kuwa katika shtaka la tatu, washtakiwa hao wanadaiwa kuisababishia hasara serikali ya Sh. milioni 75.5 kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Na. 10 (1) jedwali la kwanza na kifungu 57(1) 60 (2) kwa kutolipa tozo ya huduma, ada ya ukaguzi na mirabaha.

Katika shtaka la nne, alidai washtakiwa hao walikutwa na madini hayo kinyume cha Sheria cha Kifungu 18(1) (4) (a) cha Sheria ya Madini.

Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Edmund Kente, baada ya kusikiliza mashtaka hayo katika kesi hiyo namba 19/2023, alisema kwa kuwa kesi hiyo ni ya uhujumu uchumi, uendeshaji wake kisheria unatakiwa kupata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DDP). Aliiahirisha hadi Novemba 3 mwaka huu.

"Wote wataendelea kubaki mahabusu bila dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu Uchumi mpaka pale shauri lao litakapoitwa tena mahakamani hapa," alisema Hakimu Kante.

# Serikali yashauriwa kuongeza bajeti CMA



**Na Halfani Chusi**

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Ustawi wa Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq, ameishauri serikali kuiongeza bajeti Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati.

Toufiq alitoa rai hiyo juzi mkoani Dodoma wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya majukumu ya tume hiyo ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

"Kwa mwaka 2022/23 tumesajili kesi zaidi ya 20,156, hivyo inahitajika ipatikane bajeti ya kutosha ili ifanye shughuli zake kwa ufanisi na upana zaidi," alisema.

Alisisitiza kuwa tume hiyo ina mpango wa kuanza kujitangaza na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ili jamii iweze kutambua shughuli inazofanya.

Aliishauri tume hiyo ijifunze kutoka nchi zilizoendelea ili kupata uelewa na kujua njia rahisi wanazotumia katika utatuzi wa migogoro ya kazi.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema kuna umuhimu wa kuwa na ofisi nchi nzima zitakazoweza kurahisisha upatikanaji huduma za tume hiyo haraka na rahisi husus ani kwenye utatuzi wa migogoro ya kazi.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Cyprian Luhemeja, aliiahidi kuendelea kuisimamia CMA kwa kuzingatia ushauri na maoni ya kamati hiyo.

Awali Mkurugenzi wa CMA, Usekelege Mpulla, alisema tume hiyo imefanikiwa kutatua migogoro ndani ya siku moja hadi 30, hivyo kwa mwaka 2022/23 imesajili migogoro 20,156 kwa ngazi ya usuluhishi, sawa na asilimia 58 na ngazi ya uamuzi migogoro 8,397 sawa na asilimia 65.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO



**Na Adam Fungamwango**

# Mjane aliyeonesha njia ya kwao, wanandugu wakigawana mali

MILA ni kitu muhimu sana kwa jamii kwani huonesha mwenendo wa tabia na utamaduni wa watu wa eneo husika.

Hata hivyo kama ilivyo kwa hasi na chanya, kuna mila zingine zimepitwa na wakati, mbaya na za kukandamiza tabaka fulani ikiwamo wanawake na kuna zile ambazo hazina umuhimu wowote.

Mfano mila za kukeketa kwa sasa zinapigwa marufuku sana, huku serikali ikikaa kidete kuzitokomeza.

Kuna mila zingine ambazo zimetamalaki kwenye jamii nyingi si za Kitanzania tu, bali Afrika nzima, nazo ni za wanandugu kuchukua mali za marehemu ndugu yao na kumwacha mke na watoto wake wakitesema wasijue pa kwenda.

Miaka zaidi na zaidi iliyopita, wanawake wengi wamekuwa ni waathirika wa jambo hili, kwani wanapofiwa na waume zao, mjane analia mara mbili, kupoteza mume na kuchukuliwa mali zake.

Nimeshawahi kushuhudia mke akinyang'anywa funguo za nyumba kwenye hospitali moja kubwa hapa nchini baada ya ndugu kugundua kuwa ndugu yao aliyelazwa hapo amefariki.

Kabla ya kumweleza mkewe, walichofanya ni kumwambia awape kwanza funguo ya nyumba na baada ya hapo wakamweleza kabisa kuwa yule aliyekuwa anamwita mumewe amefariki na kwa sababu hiyo cha kufanya ni kwenda kwao tu kwani aliyemfuata sasa hayupo, kuhusu mazishi na kila kitu watajua wao, lakini mjane akapigwa marufuku hata kuhudhuria mazishi ya mumewe.

Wakati mwingine kuna ndugu wanajifanya wema, wanachukua mali na kuahidi kulea watoto wa marehemu ili wasiteseke, lakini lengo kubwa hapo ni mali tu, wakishazipata, watoto wanaanza kuteswa na hawathaminiki tena, badala yake wengine wanatoroka na kuanza kuhangaika mitaani.

Zamani sana ndugu wa marehemu walikuwa wakiwachukua na wake wa ndugu zao kuwarithi kama wake zao pia.

Mila hizi zilipungua kutokana na wengi wao kupukutika na ugonjwa wa Ukimwi, kwani baadhi ya ndugu walikuwa wakifa kwa ugonjwa huo wao hawajui wanawachukua wake wa ndugu zao na wao pia wanaupata.

Tatizo la kuwadhulumu mali wajane kama nilivyosema huko nyuma halipo hapa nchini tu, bali Afrika nzima, kwa sababu utafiti mdogo unaonyesha Waafrika ndiyo wana mila hizo.

Ndiyo maana hata mwanamuziki Madilu System alitunga na kuimba wimbo aliouita, 'Samuele Manuele', unaozungumzia madhila wanayoyapata baadhi ya kinamama wanapofiwa na waume zao.

Katika wimbo huo, Madilu ni kama mtu anayelia na kuomboleza kwenye kaburi la rafiki yake aliyefariki na kuacha familia ikiteseka baada ya ndugu kuchukua kila kitu hadi nyumba.

Analia kwenye kaburi akimwambia rafiki yake kuwa ndugu zake wamegawana kila kitu, magari, friji, nguo na jeans zake zote, lakini hawaijali familia yake.

Mkewe na watoto walikwenda kwenye nyumba aliyoiacha, lakini wakafunguliwa mbwa ambaye aliwakimbiza wakakimbia nyumba jirani.

Madilu anamwambia marehemu rafiki yake kwenye kaburi kuwa wakati alipokuwa hai familia ilikuwa na amani na furaha, ikipata karibuni kila kitu, lakini sasa inadhalilishwa na ndugu zake.

Hapa nchini mwanamuziki Cosmas Thobias Chidumule, miaka ya 1980, alitunga kibao kilichoitwa mnanionyesha njia ya kwetu, ambacho mjane anawalalamikia ndugu wa marehemu mumewe na kumwonyesha njia ya kwao, aondoke na hakuwa na kitu chochote tena pale.

"Mnanionyesha njia ya kwetu, huku mkinisimanga kuwa sina changu tena, wala faida kwenu.

Hata tanga bado halijaisha, mnaanza kugawana mali ya marehemu mume wangu hehehee, ninapouliza imekuwaje, jibu ni kwamba mnagawana mali ya mwanenu.

Mbona mmesahau, ya kuwa mali hiyo haswa, ni ya watoto wa msimamizi ni mama yao ambaye leo mnanikata.

Kama ni mila tuache, tuache kwa sababu madhara yake ni makubwa.

Mlikuwa mkiniita mke ooo, wengine shemeji ooo, wengine wifi ooo, lakini hayo mmeyasahau, kama ni msiba ni wa kweli sote, kama ni msiba mama ni wa kwetu sote.

Madhara yake ni makubwa ooo, wengine huniita shemeji ooo, wengine huniita shangazi ooo."

Kwa sasa angalau wanawake wengi wameelimika kwa kusaka haki zao.

Sms - (0716 350534)

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibuni eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry.
Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie Kwenu-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

***CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke.***

***Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibuni eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry.***

***Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake.***

***Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.***

****************************************




Kwa mbali alionekana msichana mmoja mdogo akitokea maeneo ya chini zaidi kuelekea pale alipokuwa jamaa mpya mgeni aliyekuja maeneo yale.

Kwa namna ambayo haikufahamika mara moja, ilionekana kama kila mmoja alikuwa akimtazama mwenzake.

Yule jamaa alionekana kumtazama msichana anayekuja na yeye pia alimtazama kwa makini sana.

Alipofika karibu, mgeni akavua mawani na kofia. Hakujulikana nia yake ni kutaka atambulike au vipi! Msichana akazidi kumtazama na kumshangaa. Hakuna aliyemsemesha mwenzake. Baada ya sekunde 30 hivi msichana bila kuongea neno lolote, aligeuka na kurudi mbio kurejea alikotoka.

Jamaa alitabasamu, akarudisha mawani na kofia yake kila kimoja mahala pake na kuanza taratibu kurudi alikopaki gari lake.

Alisimama kwenye nje ya gari lake kiasi cha dakika 10 hivi. Hakuna yoyote aliyepita pale alijisumbua naye.

Na hata walipomwangalia hawakumtambua. Kwa sasa alikuwa amevaa kofia na mawani juu.

Kwa mbali alianza kusikia sauti hivi. Na kweli ghafla aliona kundi la wasichana na baadhi ya wavulana wakipandisha kule alipo.

Hata hivyo walionekana kama hawajui wanayemkimbilia ni nani. Wakati wengine wakitaka kumpita na kusonga mbele, mmoja alimrukia juu na miguu yake ikabana kwenye mbavu zake na mikono kushikilia mabega yake, na yeye akimpokea kwa kumkamata mwili ili asianguke.

**Mara nyingi Sauda hugombana na kundi la rafiki za mama yake pindi anapowasikia wakimsema, au wakimteta James.**

"James, James James, James..." Yule msichana aliyemrukia aliita kwa furaha. Ndipo wenzake wakajua kumbe yule waliyetaka kumpita ndiye James mwenyewe.

Wakamzungumza na kuanza kurukaruka kwa furaha. Na kwa uthibitisho hapo hapo, alivua kofia na mawani yake waliyokuwa yameziba sura yake.

Kweli ni yeye, japo walimwona amebadilika sasa. Siyo James wanayemfahamu. Shangwe lilizidi, walirukaruka na kuimba "Amerudi, amerudi, amerudi..."

Ukweli ni kwamba vijana walifurahi sana. Walipagawa. Walichofurahi ni kumuona James ambaye kwa miaka miwili sasa hawakumwona na tayari kwa stori wanazopata kwa wazazi wao ni kwamba amefungwa jela maisha kwa kubaka, wengine amefariki kwa ajali na amezikwa na site, ili mradi tu kila mtu aliongea lake.

Hawa ni wale wanafunzi 10 ambao walijitokea kutaka kwenda kumsaka James kwenye vituo vya polisi na hospitalini baada ya kutoonekana kwa siku kadhaa alikokuwa akiishi Kinondoni Moscow, lakini hawakuruhusiwa.

Kukawa na kikundi cha watu waliozidi saba tu cha majirani waliofanya kazi hiyo lakini bila mafanikio.

Wakiwa pamoja na baadhi ya wenzao, walijitokeza kumlaki.

Hawa ni wasichana na wavulana ambao ni wanafunzi na marafiki wakubwa wa James ambao mara kwa mara alikuwa akiwasaidia kuwavusha barabara, kuwanunulia karanga na mihogo, wakati mwingine kuwasaidia wanapokutana na wanafunzi wakorofi.

Watoto hawa walijenga urafiki na imani kubwa kwa James jambo ambayo halikupendezwa sana na wazazi wao kutokana na hali ya ufukara aliyokuwa nayo.

Mpaka wakati huo, watoto waliendelea kumzunguka, kumpa mikono na wengine wakitaka hata kumbeba, lakini inashindikana kwa furaha ya kumuona.

Kwa mawazo yao ya utoto hawakuwa na haja hata ya kumshangaa kwa nini amerejea kwenye hali tofauti na ile aliyoondoka nayo. Wao furaha ya kumuona rafiki yao ndiyo ilikuwa muhimu zaidi.

Ni kweli, aliyeshuka kwenye gari hilo alikuwa ni James. Alikuja kuangalia au kuzulu eneo ambalo aliishi kiasi cha miaka miwili unusu iliyopita. Hajasahau sehemu aliyoishi kwa miaka mingi Kinondoni Moscow.

Aliteremka kwenye gari yake na kuangaza huku na huko aliangalia mandhari ya jinsi alivyoyaacha na sasa. Kulikuwa na mabadiliko kadhaa.

Akashuka chini kule ambako alikokuwa akiishi na kujionea sehemu ambayo alikuwa akiishi lililobaki gofu. Majani yalikuwa yameota zaidi na hata chumba alichokuwa akiishi, ukuta alikuwa umebomoka upande mmoja.

Wakati anashangaashangaa ndipo apomwona msichana mdogo mmoja anaitwa Salma. Ni mmoja wa wale wanafunzi rafiki zake. Hakutaka kujionyesha kwa mtu yoyote yule amtambue. Lakini alipomuona msichana yule, akakumbuka jinsi walikuwa wanamkubali na kumuonyesha upendo wa kweli tofauti na watu wengine. Akaamua ajionyeshe mbele yake. Ndipo alipovyua mawani pamoja na kofia. Akamtazama Salma ambaye aliimuangalia sana kama vile anamfananisha na mtu fulani. Alipogundua kuwa ni James, ndipo alipotoka mbio na kurejea alipotoka kwa wenzake ili awaambie amemuona James.

"James amekuja, nimemwona, yupo kule, twendeni." Alikuwa akipita nyumba moja hadi nyingine ya rafiki zake, nao pia wakaambizana wenyewe kwa wenyewe, ndiyo kisa cha kuja mbio na kumlaki wakati mwenyewe akiwa amesimama nje ya gari alilokuja nalo.

Kwa mbali kuna msichana mwingine mdogo alikuwa anakuja taratibu. Yeye alichelewa kwa sababu alikuwa anakuja taratibu wakati wenzake wanakimbia. Alipofika karibu na kundi la wenzake, akasimama. Akamtazama yule waliokuwa wanamshangilia. Hakuonekana kama ana furaha. Akasogea mbele hatua zingine kama tano hivi karibu kabisa na James. Ghafla akaanza kulia. James alimuona, akamsogelea. Wakati huo alikuwa ameshamtua Salma. Akamnyanyua na kuanza kumbembeleza. Ilikuwa kama anamzidisha. Akalia kwa sauti. Kila mmoja alijua sababu. Haya James alikuwa analia kwa sababu ya furaha iliyopitiliza ikichanganyika na kitu kama kutoamini anachokiona.

"Basi, basi Sauda, nimerudi usilie." James alimbembeleza. Kila binadamu huwa na mapokeo yake wakati kitu chochote kikimtokea. Wenzake wamempokea kwa vigelegele na shangwe. Sauda yeye alipomuona aliangua kilio.

Mara nyingi Sauda hugombana na kundi la rafiki za mama yake pindi anapowasikia wakimsema, au wakimteta James.

Furaha ya Sauda ilizidi kiasi alipomuona mwenyewe kwa macho yake, mtu ambaye alisikia akisengenywa na kikundi ya wambea ya mtaani kwao akiwemo mama yake kuwa amefungwa jela baada ya kubaka, wengine wakisema aligongwa na bodaboda akafa akazikwa na site, wapo waliosema mji umemshinda ameamua kurudi kwao kijijini.

Zile furaha za watoto zilianza sasa kuwashtua watu wazima, kuanzia kule walikotoka, njiani na hata waliokuwa eneo la tukio.

Walishangaa ni mtu gani anayeshangiliwa na kuwafanya watoto ambao wengi wao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupagawa kwa furaha namna ile?

Mpaka wakati ule hakuna mtu mzima yoyote aliyejua kuwa aliyekuwa anashangiliwa na watoto wa James yule wanayemfahamu.

Baadhi yalisikia tu jina la James, lakini hakuna alijaribu hata kuhisi kuwa atakuwa ni yule anayefahamika na watu wengi eneo lile ambaye ametoweka pale kwa miaka miwili na nusu.

***Itaendelea Jumapili***




# WASANII KUWASHA MOTO *Access Music Festival*

TAMASHA la muziki la 'Access 2023' linalotarajiwa kufanyika mara ya pili nchini litawakutanisha wasanii maarufu wa muziki duniani.

Tamasha hilo litakalofanyika kwa siku sita kuanzia Novemba 6 pamoja burudani, pia kutafanyika kongamano latakalowahusisha wasanii na wafanyabiashara wa sekta ya muziki.

Mwaka jana wasanii wengi wa Tanzania wakiongozwa na Daimond Platnumz walishiriki na kupata fursa ya kukutana na wadau mbalimbali waliopata mafanikio makubwa kwenye muziki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Music In Africa Foundation (MIAF) kutoka Afrika Kusini wanaoandaa tamasha hilo, Eddie Hatitye, amesema tamasha hilo litatoa fursa kwa wasanii wa hapa nchini kukutana na magwiji wa muziki Afrika na duniani kwa ajili ya kubadilishana ujuzi na uzoefu.

Tamasha hilo linaandaliwa na Taasisi ya Music in Africa Foundation (MIAF) litawashirikisha zaidi ya wasanii 40 kutoka Tanzania na nchi nyingine za Afrika.

"Hii ni fursa kubwa kwa wasanii wa Afrika, hasa wa hapa Tanzania, baada ya mafanikio ya tamasha la mwaka jana ambalo lilifanyika hapa wasanii watapata fursa nyingine ya kuonyesha uwezo wao na kukutana na watu waliofanikiwa kwenye muziki," amesema Hatitye.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Dk. Kedmon Mapana, amewataka wasanii wa hapa nchini kuchangamkia fursa hiyo.

"Hii ni bahati kubwa kwa tamasha kubwa namna hii kufanyika kwa mara ya pili mfululizo hapa nchini, wasanii wetu wanapaswa kuchangamkia fursa zitokanazo na uwepo wake, serikali tumetoa baraka zetu kwenye tamasha hili, tunaamini litaleta tija kwa wasanii wetu," amesema Mapana.

Mmoja wa wasanii wa Tanzania atakayeshiriki kwenye tamasha hilo, Marioo amesema wasanii watapata nafasi ya kujitangaza zaidi kimataifa na kutengeneza mazingira mazuri ya kibiashara.

"Hili ni jambo kubwa sana, ni fursa kwetu kama wasanii, nawashauri wenzangu kujiandikisha na kushirki kuweza kushiriki," anasema Marioo.

Baadhi ya watu mashuhuri watakaoshiriki ni mwanzilishi wa Symphony OS Chuka Chase (Marekani), mwanzilishi wa Roxanne Sonia, Boton-Gboh (Ufaransa), Ofisa Maendeleo wa Kimataifa wa SACEM Afrika, Akotchayé Okio (Ufaransa) na Mkurugenzi Mkuu wa Sony Music Publishing, Rowlin Naicker (Afrika Kusini).

Kwa upande wa wanamuziki watakaoshiriki wametajwa kuwa Marioo (Tanzania), Siti Muharamna na bendi ya 'The Unguja All Stars' (Tanzania), Ngwaka Son Systéme (DRC), Nour Harkati (Tunisia), Zolani Mahola & The Feminine Force (Afrika Kusini), Alostmen (Ghana), Feli Nandi (Zimbabwe), Leo Mkanyia (Tanzania), Kasiva Mutua (Kenya), Madalitso Band (Malawi), Shoo Mdjozi ( Afrika Kusini), Damian Soul, Dulla Makabila wote kutoka Tanzania.





SASA ni dhahiri mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Staa wa Bongo, Naseeb Abdul Juma amemtenga rasmi mtoto wake aliyezaa na mwanamitindo Hamisa Mobeto.

Kitu kinachoonekana hana habari na huyo, hivi karibuni Diamond ameonekana akiwa anafurahia maisha na watatu, Tiffah Dangote, Prince Nillan na Naseeb Junior.

Watoto wawili wakubwa wa mwimbaji huyo, Tiffah na Nillan, amezaa na mrembo wa Uganda Zari Hassan, wakati Naseeb Jr, amempata na staa huyo kutoka Kenya Tanasha Donna.

Siku ya Ijumaa, Diamond Platnumz alitupia mtandaoni video kionyesha watoto wake watatu wakicheza pamoja na nyingine akiwa na watoto wake wakiwa ndani ya ndege wakielekea nchini Rwanda.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NAPOLI: OSIMHEN ATAUZWA

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis amesema mshambuliaji, Victor Osimhen, 24, atauzwa huku Arsenal, Chelsea na Liverpool zikiwa na nia ya kutaka kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria. ***(Metro)***

### OSIMHEN KUMRITHI SALAH

LIVERPOOL inamwona, Victor Osimhen kama mbadala wa mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, 31, ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Saudia. ***(Mirror)***

### DAVIES ANUKIA MADRID

REAL Madrid inatazamia uhamisho wa pauni milioni 35 ili kumnunua beki wa kushoto wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies, 22 atakapoingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na mabingwa hao wa Ujerumani. ***(Bild)***

### PHILLIPS NJIA MOJA

KLABU ya Newcastle United inanakabiliwa na vita vya kuwashawishi Manchester City kumtoa kwa mkopo kiungo wa kati, Kalvin Phillips, 27, ifikapo Januari, huku Bayern Munich wakiwa tayari kuchukua hatua ya kumnunua nyota huyo wa kimataifa wa England. ***(Sun)***

### JUVENTUS YAINGIA SOKONI

JUVENTUS imeonyesha nia ya kumhitaji, Kalvin Phillips pamoja na kiungo wa kati wa Atletico Madrid na Argentina, Rodrigo De Paul, 29, kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark Pierre-Emile Hojbjerg (28). ***(Gazzetta dello)***

### ALVAREZ KUTUA MADRID

REAL Madrid inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Argentina na Manchester City, Julian Alvarez, 23 ili kuimarisha kikosi cha Carlo Ancelotti kwenye LaLiga. ***(Sebastián Srur, via Mail)***

### SPURS, WEST HAM VITANI

KLABU ya Tottenham Hotspur na West Ham zote zinamfuatilia mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, 24. ***(Teamtalk)***

### SILVA KUONDOKA CHELSEA

CHELSEA iko tayari kumruhusu mlinzi wa Brazil, Thiago Silva, 39, kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu mkataba wake utakapokamilika. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YATAJA WATATU

ARSENAL ina orodha fupi ya wachezaji wanne wanaolengwa katika dirisha la usajili la Januari, huku mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, 27, akiwa mlengwa namba moja. ***(Mirror)***

### GYOKERS MAMBO MAGUMU

SPORTING Lisbon haitamruhusu mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres (25) kuondoka isipokuwa mtu afikie kipengele chake cha kumwachilia cha euro milioni 100, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu England na Serie A zikiwa na nia ya kumnunua. ***(Record)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI ASHANGAA NACHO KUPUNGUZIWA ADHABU

**BARCELONA,** Hispania

Sasa rasmi beki huyo atakuwapo katika mechi ya Clasico...

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez amesema ameshangazwa na adhabu ya beki wa Real Madrid, Nacho Fernandez, kupunguzwa na hivyo kumfanya awe huru kucheza mechi ya Clásico wikendi ijayo.

**Nacho alitolewa nje kwa kadi nyekundu ya moja kwa moja baada ya kumchezea rafu Portu wa Girona Septemba 30, mwaka huu na awali alifungiwa kucheza mechi tatu.**

Hata hivyo, adhabu hiyo ilipunguzwa hadi mechi mbili baada ya kukata rufani wiki hii, ikimaanisha Nacho, ambaye tayari ametumikia mechi moja ya marufuku hiyo, alikosa mchezo wa jana dhidi ya Sevilla kabla ya kurejea kumenyana na Barcelona Oktoba 28, mwaka huu.

"Ni mshangao kamili," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa maoni yake juu ya uamuzi huo.

"Msimu uliopita, marufuku ya mechi tatu kwa (Robert) Lewandowski kwa kugusa pua yake haikupunguzwa, kwa hiyo ilikuwa mshangao mkubwa kuona habari za Nacho kupunguziwa hadi mechi mbili."

Kabla ya kuwakaribisha Madrid kwenye Uwanja wa Olimpiki, Barca wana mechi za nyumbani dhidi ya Athletic Club kwenye LaLiga itakayochezwa leo na wataivaa Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo Jumatano.

Wanaingia kwenye mechi hizo wakiwa na orodha ndefu ya majeruhi, ingawa Xavi alithibitisha Lamine Yamal, Alejandro Balde, Ilkay Gündogan na Ronald Araújo wote wanapatikana kumenyana na Athletic.

Pedri, Frenkie de Jong, Lewandowski, Raphinha, Jules Koundé na Sergi Roberto wote ni majeruhi na wanakabiliwa na kupona haraka tayari kuivaa Madrid.

"Ningesema inategemea ratiba na bahati mbaya wakati fulani, lakini sio kisingizio cha kutosalia na ushindani," aliongeza Xavi alipoulizwa kuhusu orodha ya majeruhi inayoongezeka.

"Araujo, Gundogan, Lamine na Balde wote wanapatikana, lakini kwa wengine itategemea hisia zao na jinsi wanavyojisikia."

Alipoulizwa kuhusu Lewandowski, Xavi alisema: "Anajisikia vizuri sana. Natumaini yuko tayari kwa Clásico. Anataka kucheza. Yeye ni kiongozi kwa maana hiyo. Daima yuko tayari kucheza hata kama kuna maumivu."

# GUARDIOLA: MESSI, HAALAND WANASTAHILI BALLON D'OR



**MANCHESTER,** England

LIONEL Messi na Erling Haaland wote wanastahili kushinda tuzo ya Ballon d'Or, kwa mujibu wa Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Messi alikuwa nahodha wa Argentina na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar huku Haaland akifunga mabao 52 katika michezo 53 na kuisaidia City kushinda mataji matatu (Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA).

Messi na Haaland ndio watu wawili wanaopendekezwa zaidi katika tuzo hiyo ambayo itatangazwa katika hafla itakayofanyika Oktoba 30, mwaka huu na Guardiola anasema wachezaji wote wawili wanastahili kushinda.

"Siku zote nilisema Ballon d'Or inapaswa kuwa katika sehemu mbili; moja kwa Messi, kisha baada ya nyingine ili Haaland ashinde," alisema Guardiola wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tulishinda tatu, alifunga mabao milioni. Msimu mbaya zaidi kwa Messi ni bora zaidi kwa wachezaji wengine. Wote wanastahili. Kiuhalisia nataka Haaland awe nayo kwa sababu alitusaidia kufikia kile tulichopata, ningependa lakini Messi alishinda Kombe la Dunia."

Haaland aliifungia Norway mabao mawili katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Cyprus wakati wa mapumziko ya kimataifa na Guardiola atatumaini itarudisha tena kiwango akiwa na City baada ya kucheza mechi tatu bila bao.

Brighton walikuwa wageni wa City kwenye uwanja wa Etihad jana.

# Henderson: Nimefuata fedha Saudia

**LONDON,** England

KIUNGO wa kimataifa wa England, Jordan Henderson (32), amekiri fedha ndio ilikuwa sababu mojawapo ya kujiunga na Al- Ettifaq ya Saudi Arabia.

Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool amesema aliumia alipozomewa na mashabiki wa England ambao hawakufurahishwa na hatua yake ya kuhamia Saudi Arabia.

Lakini amedai kumekuwa na mkanganyiko kuhusu nia ya uhamisho wake unaomfanya kulipwa mshahara wa pauni 700,000 kwa wiki baada ya kuonekana alikwenda Saudia kwa ajili ya fedha tu.


Kiungo huyo alikiambia Kituo cha televisheni cha Channel 4: "Nilifanya mahojiano miezi michache iliyopita na labda baadhi ya mambo niliyosema yalichukuliwa vibaya.


"Mfano ningesema nimekwenda Saudia sio kwa sababu ya fedha. Nadhani itakuwa tofauti kubwa sana. Sio jambo la kushangaza kwa sababu nimekwenda kwa ajili ya fedha," alisema Henderson.

Mwezi uliopita kiungo huyo aliwaomba radhi mashabiki kwa sababu anaamini amesababisha taharuki alipohamia Saudia katika dirisha la usajili la joto.

Baada ya kuichezea England mechi 80 katika historia yake ya soka alisema: "Nadhani kuwa na mchezaji kama mimi kutokana na thamani yangu itakuwa jambo zuri sana kwa Saudi Arabia.

"Kabla sijaenda Saudia thamani yangu haijabadilika, sasa wananifikiria vibaya eti kwa sababu nimekwenda nchi nyingine."





# Newcastle yaungana na Tonali

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United imethibitisha kuwa kiungo wake, Sandro Tonali anachunguzwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Italia na Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), kuhusiana na madai ya kujihusisha na kubeti, lakini wao wanamuunga mkono.

Tonali mwenye umri wa miaka 23 hivi karibuni aliondolewa kwenye kambi ya mazoezi ya Italia kutokana na kukutwa na mashtaka ya kujihusisha na kamari.

Newcastle walisema Tonali anashirikiana na mamlaka kwa uchunguzi huo: "Yeye na familia yake wataendelea kupokea uungwaji mkono kamili wa klabu. Kutokana na mchakato huu unaoendelea. Sandro na Newcastle United hawawezi kutoa maoni zaidi kwa sasa."

Tonali na mchezaji wa Aston Villa, Nicolo Zaniolo, waliondoka kwenye kambi ya Italia kwa ajili ya mechi za kufuzu euro 2024 dhidi ya Malta na England baada ya kuhusika na kubeti.

Tonali, ambaye amecheza mechi 15 kwa Italia, alijiunga na Newcastle kutoka AC Milan Julai, mwaka huu kwa uhamisho wa pauni milioni 55.

Jumanne iliopita kiungo wa Juventus, Nicolo Fagioli alifungiwa kwa miezi saba na FITC kwa kukiuka sheria za kamari huku pia akipigwa faini ya euro 12,500.

HABARI MICHEZO

## Mshindi wa CRDB akabidhiwa gari

Na Maria Seme

MKAZI wa Dar es Salaam, Alex Bakunda, ameibuka mshindi wa nne wa zawadi ya gari aina ya Toyota Crown kwa mwezi huu katika kampeni ya Benki ni Simbanking inayoendeshwa na Benki ya CRDB.

Bakunda anayetumia programu za kampuni tofauti kupata huduma amesema SimBanking App ya CRDB ni nzuri na ndio maana amekuwa anaitumia mara kwa mara kukamilisha miamala yake.

"Kuna siku nilisafiri nje ya nchi halafu nikatakiwa kufanya malipo fulani, jambo ambalo liliniumiza kichwa kwa kuwa sikuwa na namna kabla kutumia SimBaking inaweza kufanikisha hilo, nilipoitumia, kweli ilinisaidia na nikatatua changamoto hiyo," alisema Bakunda.

Kuhusu kushinda gari, Bakunda alisema wakati anapigiwa simu, alishindwa kuipokea kwa sababu alikuwa kwenye mkutano, lakini ilipoita tena akaona aipokee kujua ni nani anayemtafuta kwa namba ngeni.

"Nilidhani ni wale jamaa (matapeli). Ni furaha kwangu leo (jana), kulipokea gari hili, ninawaomba Watanzania wenzangu tutumie huduma za benki hasa hizi za kidijiti kwani uwezekano wa kushinda kwenye kampeni kama hii ya "Benki ni SimBanking" inayoendeshwa na CRDB ni mkubwa," alisisitiza.

Bakunda anaungana na Robert Masala aliyeibuka kidedea Julai na kupewa Toyota Crown huku Jared Awando Ojweke alikishinda Mei na Mayani Yahaya Hassan aliyekuwa wa kwanza.

Akimkabidhi gari hilo, Mkuu wa Idara wa Wateja Binafsi wa CRDB, Stephen Adili alisema Bakunda alistahili zawadi hiyo kwa kuwa droo ilipochezeshwa namba mbili zilizochaguliwa kwanza hazikupokewa mpaka yeye aliyechaguliwa mara tatu ndio alipokea.

"Utaratibu unataka namba iliyochaguliwa ipigwe mara tatu. Tulifanya hivyo kwa namba ya kwanza na ile ya pili nayo tukaipiga mara tatu, zote hazikupokewa. Bakunda naye hakupokea simu yake ilipoita mara mbili lakini baadaye alipokea, hakika wewe ulistahili ushindi huu," alisema.

# MFUGALE AZINDUA RASMI KILI MARATHON 2024 DAR

Na Mwandishi Wetu

MSIMU wa 22 wa mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Marathon 2024 umezinduliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam, imefahamika.

**Mbio za Kilimanjaro zimepangwa kufanyika Februari 25, mwakani 2024.**

Akizungumza jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Utalii, Damas Mfugale ambaye alikuwa mgeni wa heshima, alipongeza mafanikio ambayo yameshafanyika hadi sasa kwa mchango wa kutangaza utalii wa michezo.

"Tunaona fahari ya Mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon kwa sababu zimethibitisha ni moja ya matukio makubwa ya kimataifa katika mkoa kwa vile yamewaleta pamoja washiriki zaidi ya 12,000 na idadi sawa ya watazamaji kutoka zaidi ya nchi 56 na wote hawa wanaweza kuwa watalii. Haya ni mafanikio makubwa.

Ni wakati sasa Bodi ya Utalii Tanzania iimarishe uhusiano na mbio hizi kwa kutafuta njia zaidi za kutangaza utalii wa michezo kwa vile ni wazi kwamba tukio ni jukwaa kubwa na lina wafuatiliaji wengi ndani na nje ya nchi," alisema Mfugale.

Ofisa huyo pia aliwasihi washiriki na watazamaji kutumia msimu wa Kilimanjaro International Marathon kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii kikiwamo kivutio kikubwa zaidi ambacho ni Mlima Kilimanjaro, Serengeti, Ngorongoro, Zanzibar na vivutio vingine. Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TBL Group, Jose Moran wa kampuni inayozalisha, usambazaji na kuuza bia mbalimbali na vinywaji visivyo na kilevi Tanzania, alisema wanaona fahari kudhamini mbio hizo kwa miaka 22.

Moran alisema wametenga kiasi cha fedha zipatazo Sh. milioni 28 kwa ajili ya tuzo, ambapo washindi wa juu katika makundi yote mawili ya wanaume na wanawake, kila mmoja atapata zawadi ya Sh. milioni tano.

Aliwataka washiriki kujisajili kwa muda unaotakiwa kupitia www.kilimanjaromarathon.com na kupitia TigoPesa.

Meneja wa Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael ambaye kampuni yake inafadhili mbio za nusu marathon alisema; "Kama sehemu ya kujitoa kwetu kutangaza utalii wa michezo Tanzania na kulea vipaji vya wanariadha, tunafurahi kutangaza Tigo ni mdhamini wa mbio hizo kwa miaka tisa mfululizo.

Shisael alisema ubunifu wao wa namna ya washiriki kujisajili kupitia simu umesaidia kuongeza washirirki na kuongeza mchakato huo ufanyika kwa kupiga *150*01#, halafu kubonyeza 5 LKS, kisha kubonyeza 5 (tiketi) na kufuata maelekezo kukamilisha usajili.

Alisema mwisho wa zoezi la kujisajili Desemba 14 na baada ya hapo ada ya kiingilio itaongezeka katika makundi yote na mataifa yote na dirisha rasmi litafungwa Februari 5, mwakani.

Mbio za Kili International Marathon 2024 zitafanyika Februari 25, mwakani kwenye Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU), zinaandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Marathon na kuratibiwa na Kampuni ya Executive Solutions.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania, Stephen Mpeka (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi mbio za Kili International Marathon 2024 ambazo zitafanyika Februari 25, mwakani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## 'Hongera Tanzania'

INATOKA UK. 24

ngumu lakini walipambana na kupata sare mbele ya timu bora kwa Afrika.

"Ulikuwa mchezo mzuri sana na mgumu kwa kila timu, tumepata sare nyumbani na tunajipanga kwa ajili ya mechi ijayo, tunaenda kupambana na tutajitahidi tuwezavyo kusaka matokeo mazuri Misri," alisema Chama.

Kocha wa Al Ahly, Marcel Koller alisema mechi ilikuwa ya kimbinu na ufundi kwa sababu kila timu imecheza kwa vipindi, wao walitawala kipindi cha kwanza na Simba iliwashika kipindi cha pili.

Alisema kipindi cha kwanza walitengeneza nafasi nyingi za wazi na lakini walishindwa kuzitumia huku makosa waliyofanya kipindi cha pili yaliifanya Simba kuwa bora.

"Tulikosa penalti, nadhani ni uamuzi wa mwamuzi, niwapongeze Simba kipindi cha pili walicheza vizuri, kutoka nyuma na kusawazisha kila bao, hatukucheza vizuri kipindi hicho tunaenda kujipanga kwa mchezo wa marudiano nyumbani," alisema kocha huyo.

## Yanga, Azam kamili kumalizana

INATOKA UK. 24

"Uwanja wa Azam Complex umekuwa na bahati kubwa kwetu, ni zaidi ya uwanja wetu wa nyumbani, tulikuwa hatuna wasiwasi hata kidogo kucheza mechi kwenye uwanja ule, lakini kwa kutambua hamu ya mashabiki wetu, kutambua idadi kubwa ya mashabiki wetu ambao wamekuwa wakikosa kuiona timu kutokana umbali, ufinyu na udogo wa uwanja wenyewe, " Haji.

Kuhusu maandalizi ya mechi hiyo, bosi huyo alisema hakuna mechi rahisi katika ligi kwa sababu wanaenda kukutana na Azam ambayo ina kikosi kizuri na ni moja ya timu chache ambazo lengo lao pia ni kutwaa ubingwa.


Aliongeza kikosi chao kitashuka dimbani kikiwa imara na hawatabwetesha na matokeo ambayo walipata Tanga katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ngao ya Jamii.

Msemaji wa Azam FC, Hasheem Ibwe, ameliambia Nipashe wachezaji wote wa timu hiyo wana ari kubwa ya kusaka ushindi na wameahidi kumaliza 'uteja' kwa mabingwa hao watetezi.

# Michezo

Jumapili Oktoba 22, 2023

Nipashe

Newcastle yaungana na Tonali UKURASA 22



Rais wa FIFA, Gianni Infantino (katikati) na Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger wakiwa na wachezaji na benchi la ufundi la Simba baada ya kumalizika kwa mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League dhidi ya Al Ahly ya Misri iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga, Azam FC kamili kumalizana

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamesema licha ya mchezo wao wa kesho dhidi ya Azam FC unatarajiwa kuwa mgumu, wanaahidi kuwapa furaha mashabiki wao na kuendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Yanga pia imefurahia mabadiliko ya uwanja ambapo sasa mchezo huo utafanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam badala ya Azam Complex, kama ilivyotangazwa hapo awali.

Baada ya kukamilisha kwa maboresho, Uwanja wa Benjamin Mkapa ulifunguliwa rasmi juzi kwa mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League iliyowakutanisha wenyeji Simba dhidi ya Al Ahly kutoka Misri, mchezo uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Akizungumza na gazeti hili, Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema klabu imefurahi kuona timu inarejea kwenye Uwanja wa Mkapa kwa sababu anaamini wanachama na mashabiki wengi wa timu hiyo watapata fursa kuhudhuria mchezo huo bila kuhofia umbali na ufinyu ambao wangeupata Chamazi.

INAENDELEA UK. 23

# Infantino: Hongera Tanzania

**Na Saada Akida**

## ●●● Robertinho aahidi kuivaa Al Ahly tofauti ili...

WAKATI Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Gianni Infantino, akipongeza Tanzania kwa mafanikio ambayo imeyapata katika mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Robert Oliviera 'Robertinho', amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake ilipocheza dhidi ya Al Ahly kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

**Mechi hiyo ya ufunguzi ya michuano ya African Football League ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2, Simba ikienda mapumziko ikiwa nyuma kwa bao 1-0.**

Akizungumza wakati ameenda kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Michezo cha kinachomilikiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kilichoko Kigamboni jijini, Infantino alisema kupitia soka Tanzania imefanikiwa kuiunganisha dunia.

Infantino alisema kauli ya mpira unaunganisha dunia, imejidhihirisha kwa vitendo hapa Tanzania na itabakiwa kuwa kumbukumbu chanya kwa vizazi vijavyo pamoja na serikali.

"Asante sana Wallace (Karia), kaka yangu Patrice (Motsepe), marais wote vya vyama vya michezo, wachezaji wakongwe, tunajivunia kwa nafasi ambayo umetupa ya kuwa hapa leo (juzi), tunajivunia kushuhudia mradi huu wa Kigamboni na Tanga, ni mradi ambao utasaidia maendeleo ya soka. Kila nchi duniani inapokea fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, miradi ambayo inatakiwa itumike kwa uwazi, Tanzania ni baadhi ya nchi ambazo zimetekeleza hilo, hongera sana, tunashukuru pia mashindano haya (AFL), yameanza na yameanzia Tanzania. Yameunganisha dunia," alisema Infantino.

Bosi huyo pia aliwashukuru marais wote wa vyama vya soka kutoka mataifa mengine waliofika Tanzania, wachezaji wakongwe pamoja na wadau wengine muhimu.

Naye Robertinho amewapongeza nyota wake kwa kuonyesha kiwango bora katika kipindi cha pili na aliweka wazi mabadiliko aliyofanya yaliimarisha idara ya kiungo na kufunga mabao mawili.

Kocha huyo alisema haikuwa mechi rahisi rahisi kwa kuwa Al Ahly ni timu bora Afrika hasa inapokuwa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mipango yake ni kuhakikisha anashinda mechi ya marudiano itakayochezwa Misri.

Alisema Al Ahly timu bora na yenye uzoefu na michezo mikubwa, inapiga pasi fupi fupi na wanafanya mashambulizi ya kushtukiza ambayo wanapaswa kuongeza umakini ili kupunguza makali yao.

"Kila mchezo una mipango yake, leo (juzi) tulipanga kucheza hivi na wachezaji wangu walijitahidi kuonyesha uwezo, Simba imesajili nyota 28, hao wote huwezi kuwatumia pamoja katika mechi moja, wachezaji wanapangwa kutokana na aina ya mechi.

Leo (juzi) hatukuwa na namba tisa lakini Baleke, Bocco na Phiri walikuwa benchi kutokana na aina ya mechi iliwahitaji zaidi viungo kuliko washambuliaji, mchezo ulikuwa mzuri kwa kila timu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa hawezi kuzungumzia mchezo ambao hawajacheza lakini malengo ya Simba ni kushinda ugenini na kusonga mbele katika mashindano hayo.

"Nimeona mapungufu yaliyojitokeza katika mechi hii, tunarudi uwanjani kufanyia kazi kujiandaa na mchezo wa marudiano utakaochezwa Misri Oktoba 24, mwaka huu," alimaliza Mbrazil huyo.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein (Zimbwe Jr), alisema kulingana na walivyocheza anaimani watafanya vizuri katika mchezo wa marudiano na kufikia malengo.

"Nafasi bado tunayo ya kusonga mbele, muhimu ni kushirikiana kwa pamoja katika kujiandaa na mchezo wa marudiano, tutakwenda kufanya vizuri ugenini," alisema Zimbwe Jr.

Kiungo wa Simba, Clatous Chama alisema mechi ilikuwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >